# Nipashe

Jumamosi Februari 22, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580161

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US




## Jamhuri yatwishwa zigo kuhusu kukamatwa Lissu

UKURASA 3




UKURASA 13

# NI MSHTUKO

• **Lugola**, wenzake kushtakiwa madai ya uhujumu uchumi, uchunguzi wakamilika, jalada kutua kwa DPP... *Endelea ukurasa 2*



Aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Ndani, Kangi Lugola (kulia) na aliyekuwa Kamishna Jenerali wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Thobias Andengenye, wakijadiliana jambo wakati wakitekeleza majukumu ya ujenzi wa taifa jijini Dar es Salaam, kabla ya kutenguliwa nyadhifa zao. **PICHA: MAKTABA**

## Kigogo wa Takukuru amwomba DPP yaishe

UKURASA 3





Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store


## JPM achangiwa fedha kuchukua fomu ya urais

UKURASA 2


**MICHEZO** **SIMBA KUNOGA TENA TAIFA LEO** UK.32

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Mshituko kina Lugola kushtakiwa uhujumu

Na Romana Mallya

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), imesema uchunguzi wa tuhuma zinazomkabili aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola, na wenzake umekamilika na imeona zinaangukia kwenye makosa ya uhujumu uchumi.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu Takukuru, Brigedia Jenerali John Mbungo, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu uchunguzi wa mkataba wa makubaliano kati ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji na Kampuni ya Rom Solutions wenye thamani ya zaidi ya Sh. trilioni moja.

Uchunguzi huo unatokana na maagizo yaliyotolewa hivi karibuni na Rais John Magufuli baada ya kubaini kile alichokiita utata katika utekelezaji wake.

Mbali na Lugola, ambaye pia ni Mbunge wa Mwibara mkoani Mara, kashfa hiyo pia inamgusa aliyekuwa Kamishna Jenerali wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Thobias Andengenye, na maofisa wengine 15 wa serikali.

Jenerali Mbungo alisema uchunguzi wa Takukuru kuhusu jalada hilo umekamilika kwa asilimia 99.9 kwa sababu ushahidi muhimu dhidi ya tuhuma hizo umepatikana.

"Ushahidi muhimu umepatikana na kilichobaki ni taratibu za uwasilishaji wa jalada hili la uchunguzi Ofisi ya Taifa ya Mashtaka. Tutaliwasilisha jalada hili katika ofisi hiyo ndani ya wiki moja kuanzia sasa (jana saa nane mchana)," alisema.

Bosi huyo wa Takukuru alisema kwa ujumla watuhumiwa wako 17 na kwamba wanaendelea kuitwa na kuhojiwa kwa sababu wako nyumbani kwao.

Alisema Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) atakavyoona inafaa kupelekwa mahakamani, watuhumiwa hao wataitwa na kwamba uchunguzi wao ulilenga kuthibitisha iwapo kuna uwezekano watumishi kuwa wamezembea na kutokuzingatia sheria.

"Tuliangalia kama kuna vitendo vya rushwa au waliosaini kama walikuwa na uhalali wa kisheria wa kufanya hivyo, kampuni husika ilikuwa na uhalali wa kisheria kuingia zabuni? Kingine ni kama kuna ukwepaji wa kodi. Tulichunguza kama kuna matumizi mabaya ya madaraka," alisema.

Jenerali Mbungo alisema makosa yote hayo aliyoyachunguza yameangukia kwenye makosa ya uhujumu uchumi.

"Baraza lilitakiwa lipewe taarifa, Waziri alitakiwa apeleke ombi kwenye baraza nalo limshauri Rais. Bunge lilitakiwa lipitishe. Haya yote hayakufanyika ndiyo maana tunasema mkataba huu ni batili.

"Mkataba ulivyo, haukufuata utaratibu wowote wa serikali, cha kwanza ni kuvunja na kuufuta, wahusika wameshawasilisha ombi la kuuvunja mkataba na hawatadai chochote serikalini," alifafanua.

Alisema kila tukio la uhalifu lina mazingira yake na lina aina yake ya watu waliofanya tukio lile la uhalifu.

"Kwa nini hawa wako nje na wengine wapo ndani? Ni swali zuri. Tunachofanya ni uchunguzi wa tukio, upande wa pili ni suala linalohusiana na intelijensia ikiwamo uwezo wa kutoroka kutokana na ukubwa wa kosa. Intelijensia ikituambia huyu mtu anaweza kutoroka tunawatafuta," alimjibu mmoja wa waandishi wa habari.

Kiongozi huyo wa Takukuru alibainisha kuwa taasisi hiyo inayo majina ya watuhumiwa zaidi ya saba ambao wametoroka nchini akiwamo wa Pride International, mwanamke aliyejipatia mali nyingi bila maelezo yoyote, na walitapeli zaidi ya dola za Marekani milioni 20 ili kuanzisha kiwanda cha saruji Lindi na kudhaminiwa na serikali, wakapata mkopo.

"Hawa wote tunaowachunguza sasa hivi wote ni watumishi wa serikali, uwezekano kwamba watakimbia hatuuoni na inasaidia kitu kimoja, siyo busara ukawarundika watu kwenye mahabusu zetu ambazo zimejaa sasa hivi kama kuna uwezekano wa huyu mtu kupatikana kila wakati anapohitajika.

"Uchunguzi unaangalia pande zote, hii ni kazi inayozingatia taaluma ya uchunguzi, ni kazi inayoongozwa na weledi wa kiuchunguzi na kiintelijensia.

"Ninajua wapo watu wanaongea kitu ninachokisema na wanatolea mifano ya Uingereza, Marekani kwamba mtu hakamatwi mpaka uchunguzi ukamilike, siyo kwetu hapa, wenzetu ni mifumo iliyoendelea kutoroka mhalifu Marekani siyo kitu rahisi, utatoroka dakika mbili umekamatwa lakini hapa tunawatafuta watu saba mpaka leo," alisema.

## Baba kortini tuhuma za kulawiti mtoto

Na Daniel Limbe, CHATO

JESHI la Polisi wilayani Chato mkoani Geita, limemfikisha mahakamani Kazimili Dotto, akituhumiwa kumbaka na kumlawiti mtoto wake wa kambo, ambaye ni mwanafunzi wa darasa la pili.

Mshtakiwa huyo ambaye ni mkazi wa Kijiji na Kata ya Makurugusi wilayani hapa, anadaiwa kumbaka na kumlawiti mtoto wa mkewe na kutishia kumuua kwa kisu iwapo angesema kutendwa ukatili huo.

Katika Mahakama ya Wilaya ya Chato, Mwendesha Mashitaka wa Polisi, Mauzi Lyawatwa, alidai mshitakiwa anakabiliwa na kosa la ubakaji ambalo ni kinyume cha kifungu cha 130(1)(2)(e) na 131(1) cha Sheria ya Makosa ya Jinai.

Alidai kuwa Februali 17 mwaka huu, majira ya mchana, mshitakiwa akiwa nyumbani kwake, alimwita mtoto huyo na kumwomba amletee maji ya kunywa ndani ya chumba anacholala na mkewe kabla ya kumbaka na kumlawiti.

Alidai kuwa baada ya mtoto huyo (jina tunalihifadhi) kufikisha maji, alikamatwa kwa nguvu na kutupiwa kitandani na baba yake kisha kumvua nguo za ndani na kuanza kumbaka na kumlawiti.

Ilidaiwa mahakamani hapo kuwa wakati hayo yakifanyika, mama wa mtoto alikuwa shambani na aliporejea, alisukuma mlango wa chumba chake uliokuwa umeegeshwa, kisha kumfumania mumewe akiwa kifuani kwa mtoto wao huku wote wakiwa hawana nguo.

Alidai kuwa baada ya kuona hali hiyo, aliamua kupiga yowe kuomba msaada na majirani walipofika, waliamua kuita askari wa Jeshi la Polisi, ambao walifika na kumweka mshitakiwa chini ya ulinzi.

Baada ya kutolewa maelezo hayo na Upande wa Jamhuri, mshitakiwa alikana kuhusika na mashtaka yanayomkabili.

Hakimu Mkazi Mfawidhi Odira Amworo, aliahirisha kesi hiyo hadi Februali 24 mwaka huu.



Mwenyekiti wa Chama cha Ushirika cha Mkoa wa Arusha (ACU), Bethuel Akyoo (kushoto) na wenzake, wakipandishwa kwenye gari la polisi, jijini Arusha jana, baada ya kukamatwa kwa tuhuma za ubadhirifu wa zaidi ya bilioni 4, mali ya wanachama. **PICHA: ASRAJI MVUNGI**

# JPM achangiwa fedha kuchukua fomu urais

Na Woinde Shizza, ARUSHA

JUMUIYA ya Wazazi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) mkoani Arusha, jana ilimkabidhi Mwenyekiti wa jumuiya hiyo Taifa Sh. milioni moja kwa ajili ya kumchukulia Dk. John Magufuli fomu ya kuwania nafasi ya urais kwa awamu ya pili.

Akizungumza wakati wa makabidhiano hayo, Katibu Mwenezi wa Wilaya ya Arumeru, Joshua Ongura, alisema kutokana na tamko la Mwenyekiti wa jumuiya hiyo Taifa la Desemba mwaka jana wakati wa kongamano lao jijini Dar es Salaam, wameona watoe fedha hizo.

Alisema katika kongamano hilo, Jumuiya ya Wazazi iliahidi kumchukulia Dk. Magufuli fomu ya kugombea urais kwa awamu ya pili.

Alisema kwa kuwa Mkoa wa Arusha unaanzia na alama A, wameamua kuwa wa kwanza kumchangia Rais na pia wameona watoe fedha hizo kutokana na namna alivyotekeleza vyema ilani ya chama na kutatua matatizo ya wananchi.

Baada ya kukabidhiwa fedha hizo, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi Taifa, Edmond Mndolwa, aliwashukuru kwa moyo walioonyesha kwa Rais Magufuli.

Alisema iwapo mikoa yote itatoa fedha hizo, zitapatikana Sh. milioni 31 ambazo kati yake, watachukua Sh. milioni moja na kumchukulia fomu Rais na zitakazobaki wataifanyia kampeni.

Aliitaka mikoa mingine kuiga na kuanza kumchangia fedha kwa ajili ya fomu Rais ili kufanikisha lengo lao hilo.

# Kigogo wa Takukuru amwomba DPP yaishe

**Na Hellen Mwango**

MCHUNGUZI Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Cosmas Batanyika, ameiomba Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu kukutana na kamati inayoshughulika na kukiri na kuomba msamaha kwa makosa ya uhujumu uchumi.

Batanyika (44) anakabiliwa na tuhuma za kushawishi rushwa ya zaidi ya Sh. milioni 300, kupokea na kutakatisha Dola za Marekani 20,000.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, alidai jana mbele ya Hakimu Mfawidhi, Godfrey Isaya, kuwa kesi hiyo imekuja kwa ajili ya kutajwa na kwamba upelelezi bado haujakamilika.

Baada ya kueleza hayo, Batanyika aliiomba mahakama kukutana na kamati ya inayoshughulika na kukiri na kuomba msamaha kwa makosa ya uhujumu uchumi.

Wakili Simon alidai atafikisha kilio chake kwa kamati hiyo ili kukutana nayo.

Baada ya kueleza hayo, Hakimu Isaya aliahirisha kesi hiyo hadi Machi 6, mwaka huu, kwa ajili ya kutajwa. Katika mashauri yaliyopita, mshitakiwa huyo aliieleza mahakama kuwa amemwandikia barua Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) kwa ajili ya kukiri na kuomba msamaha kwa makosa yake.

Katika mashtaka ya kwanza inadaiwa Februari 9, mwaka jana, eneo la Upanga, mshtakiwa akiwa mwajiriwa na Takukuru katika nafasi ya Mchunguzi Mkuu, aliomba rushwa ya Sh. milioni 200 kutoka kwa Hussein Gulamali Hasham kwa lengo la kuharibu ushahidi wa tuhuma za kukwepa kodi zilizokuwa chini ya uchunguzi wa mwajiri wake.

Ilidaiwa kuwa Februari 10, mwaka jana katika Viwanja vya Maonyesho ya Biashara ya Sabasaba, Temeke jijini Dar es Salaam, alijipatia Dola za Marekani 20,000 kutoka kwa Faizal Hasham kama kishawishi cha kuharibu ushahidi wa tuhuma za kukwepa kodi dhidi ya Hussein Gulamali Hasham zilizokuwa zinafanyiwa uchunguzi na Takukuru.

Pia ilidaiwa kuwa Februari 13, mwaka jana, katika ofisi za Makao Makuu ya Takukuru, mshtakiwa akiwa mwajiriwa na Mchunguzi Mkuu wa Takukuru, alishawishi rushwa ya Dola za Marekani 50,000 kutoka kwa Thangavelu Nallavan Vall kama kishawishi cha kuharibu ushahidi wa tuhuma zilizokuwa zinamkabili za kukwepa kodi.

Katika mashtaka ya nne, ilidaiwa kuwa Februari 14, mwaka jana, katika mtaa wa Haile Selasie karibu na Merry Brown, Kinondoni, alishawishi rushwa ya Dola za Marekani 20,000 kutoka kwa Nallavan Vall kama kishawishi cha kuharibu ushahidi uliokuwa chini ya uchunguzi wake dhidi ya kukwepa kodi.

Pia Februari 10, mwaka jana, eneo la Sabasaba, mshtakiwa akiwa mwajiriwa na Mchunguzi Mkuu wa Takukuru, alipokea Dola za Marekani 20,000 wakati akijua ni zao la kutakatisha na zimetokana na rushwa.

Katika mashtaka ya sita, ilidaiwa kuwa Februari 19, mwaka jana, eneo la Village Super Market katika duka la kubadilishia fedha za kigeni la Electron, mshtakiwa alibadilisha sehemu ya Dola za Marekani 7,000 na kupata Sh. milioni 16.1 kati ya 20,000 huku akijua ni zao la rushwa.

Katika mashtaka ya saba, ilidaiwa kuwa Februari 19, mwaka jana eneo la Chamazi Wilaya ya Temeke, Dar es Salaam, mshtakiwa alinunua ardhi eneo ambalo halijapimwa lenye thamani ya Sh. milioni 15.8 huku akijua fedha hizo ni za kutakatisha na ni zao la rushwa.

Mshitakiwa hakutakiwa kujibu chochote kwa sababu mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi za uhujumu uchumi na mshtakiwa alirudishwa rumande ambako yuko mpaka sasa.



Mkurugenzi wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini katika Wizara ya Afya, Idara Kuu Maendeleo ya Jamii, Prudence Constantine, akizungumza na waadishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu maadhimisho ya kitaifa ya Siku ya Wanawake Duniani yatakayofanyika jijini Dodoma tarehe 27 mwezi huu. Kushoto ni Ofisa Maendeleo ya Jamii Mkuu wa Wizara hiyo, Idara kuu ya Maendeleo ya Jamii, Erasto Ching'oro. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Jamhuri yatwishwa zigo kukamatwa Lissu

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam, imetoa siku 14 kwa upande wa Jamhuri kujibu maombi ya wadhamini wa Mbunge wa zamani Singida Mashariki, Tundu Lissu, kwamba wameshindwa kumpata ili mahakama itoe amri ya kumkamata.

Wadhamini hao, Robart Katula na Ibrahim Ahmed, kwa nyakati tofauti jana waliieleza mahakama kuwa wamewasilisha maombi wakiomba mahakama itoe hati ya kukamatwa kwake ili wajitoe udhamini kutokana na mtuhumiwa huyo kutohudhuria kesi yake.

Amri hiyo ilitolewa na Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba, baada ya upande wa Jamhuri kukiri kupokea maombi hayo na kwamba wanaomba muda wa kuyajibu.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, alidai kuwa upande wa Jamhuri umepokea maombi yaliyoambatanishwa na hati ya kiapo lakini wanaomba muda wa kutosha kuyachambua.

Hakimu Simba alisema mahakama yake inatoa siku 14 kwa upande wa Jamhuri na kuwasisitiza watumie siku 10 kuhakiki maombi hayo kabla ya kurejea mahakamani.

Katika kesi ya msingi, Hakimu Simba, aliwataka wadhamini kueleza alipo mshtakiwa Lissu kwa kuwa walishakiri kwamba amepona na mahakama ilihitaji kumwona akihudhuria kesi.

Mmoja wa wadhamini hao, Katula, alidai kuwa ni kweli alisema mshtakiwa amepona lakini walipojaribu kuwasiliana naye ili aje mahakamani alidai ana wasiwasi na usalama wa maisha yake ndiyo maana ameomba mahakama ishughulikie maombi yao.

Kabla ya hakimu kupanga tarehe, Wakili Simon alidai kuwa mshtakiwa namba mbili katika kesi hiyo,

Simon Mkina, hakuonekana mahakamani kwa siku mbili bila taarifa, hivyo akaiomba mahakama itakaporudi mshtakiwa aonywe na wadhamini wake watoe maelezo ni kwa nini mshtakiwa hakuhudhuria mahakamani.

Akijibu hoja hiyo Wakili wa Utetezi, Nyaronyo Kicheere, alidai kuwa jana Mkina alifika lakini aliumwa ghafla akalazimika kurudi nyumbani na bado hali yake si nzuri.

Hakimu Simba aliendelea kusisitiza wadhamini wa Lissu kumleta mahakamani hapo kwa kuwa amri za kesi hiyo bado zinaendelea mpaka zitakapotenguliwa baadaye. Kesi hiyo imeahirishwa mpaka Machi 10, 2020.

Lissu na wenzake wanne katika kesi ya msingi wanakabiliwa na mashtaka matano ikiwamo kuandika habari za uchochezi kinyume na Sheria ya Magazeti ya Mwaka 2002.

Ilidaiwa kuwa kati ya Januari 12 hadi 14, 2016 jijini Dar es Salaam, washtakiwa Jabir Idrisa, Mkina na Lissu, waliandika na kuchapisha taarifa za uchochezi zenye kichwa cha habari kisemacho, 'Machafuko yaja Zanzibar.'

Katika shtaka la pili, wanadaiwa kuwa Januari 14, 2016 walichapisha habari hizo ili kuleta chuki kwa wananchi wa Zanzibar.

Mshtakiwa Mehboob anadaiwa kuwa Januari 13, 2016 katika jengo la Jamana lililopo Manispaa ya Ilala, alichapisha gazeti la Mawio lililokuwa na taarifa za uchochezi.

Ilidaiwa kuwa mshtakiwa huyo pia alichapisha gazeti hilo bila ya kuwasilisha hati ya sheria ya kiapo kwa Msajili wa Magazeti.

# Wavuvi wasusia kikao cha DC

**Na Jovither Kaijage,** UKEREWE

MKUU wa Wilaya ya Ukerewe mkoani Mwanza, Cornel Magembe , amelazimika kuahirisha kikao chake na wadau wa uvuvi hadi Jumanne kutokana na mwitikio hafifu wa wajumbe wa kikao hicho.

Akizungumza jana wakati akiahirisha kikoa hicho, Magembe alisema idadi ndogo ya waliofika kwenye kikao hicho ni sababu ya kutofanyika.

"Ndugu zangu nimealika Mbunge, Mwenyekiti wa Halmashauri na Mwenyekiti wa CCM Wilaya pamoja na wakuu wa idara na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ili tuwasikilize na kutatua kero zenu. Lakini kama mahudhurio ndiyo haya, suala hili naachana nalo na tusilaumiane," alisema.

Hata hivyo, kabla ya kuahirisha kikoa hicho, alitoa fursa kwa wajumbe 35 kati ya 125 waliotarajiwa kuhudhuria, watoe maoni yao ambapo wengi walikubali kiahirishwe na kutofautiana na katibu wa umoja wao, Paul Mayunga, aliyetaka kiendelee.

Katibu wa umoja wa wavuvi wa visiwa 17 vya kata ya Ilangala, Manyunga, akitetea hoja yake, alisema wavuvi katika visiwa hivyo wamekutana na wametuma wajumbe watakaowakilisha mawazo yao.

Davis Mkama, mvuvi wa kisiwa cha Malelema, akionyesha kutoridhishwa na mahudhurio, alisema wavuvi wanakabiliwa na matatizo mengi, hivyo ni vyema wakapata fursa ya kushiriki na kutoa kero zao.

"Ndugu DC nakushauri utuvumilie na uache hasira. Sisi ni wananchi wako nakuomba upange siku nyingine ili tukutane na hata ikibidi gharama za kikao hicho kama za chakula na ukumbi ziwe za kwetu kwa sababu sisi ndio wenye shida," alisema Mkama.

Benson Mboya, mvuvi wa kisiwa cha Kamasi, alisema kitendo cha wadau wa sekta hiyo kususia kikao hicho ili kupata suluhu ya matatizo yao ni unafiki na kushindwa kutambua fursa za kutatua kero zao.

"Nakubaliana na hoja yako kuahirisha kikao ili twende tukajipange upya ili wadau wengi wapate fursa ya kueleza yanayowasibu ikizingatiwa zipo kero nyingi. Mbali na wadau wengi kuumizwa kiuchumi katika kipindi cha operesheni ya kudhibiti uvuvi haramu pia wamependishiwa ushuru na kodi hali ambayo inasababisha washindwe kumudu gharama za kuendesha shughuri zao," alisema.

Mbunge wa Ukerewe, Joseph Mkundi, akionekana kusikitishwa na hatua ya wavuvi kushindwa kujitokeza kueleza kero zao, alisema alitegemea kupata mawazo mapya na tofauti ambayo yangemsaidia kipindi hiki ambacho mchakato wa kuifanyia marekebisho Sheria ya Uvuvi ya mwaka 2003 unaendelea.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Goerge Nyamah, akizungumzia suala hilo, alitaka kikao hicho kipangiwe siku nyingine kwa maelezo pengine hali ya mawasiliano ya mwaliko haikuwa nzuri.

# Wabunge mtegoni kwa kukacha kikao cha CCM

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

KATIBU wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Shinyanga, Donald Magesa, ameagiza wabunge wote wa CCM mkoani hapa kuandika barua kujieleza kwa nini hawajahudhuria kikao cha Halmashauri Kuu ya CCM Mkoa.

Magesa alisema hayo jana kwenye kikao hiocho kilichokuwa na lengo la kusoma taarifa ya utekelezaji ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM kuanzisha Januari, 2016 hadi Desemba, mwaka jana.

Alisema haiwezekani baadhi ya wabunge wa mkoa huo wasiwapo kwenye kikao hicho bila ya kutoa taarifa yoyote wakati wao ni wajumbe muhimu wa utekelezaji wa ilani hiyo. "Naagiza makatibu wa wilaya wa CCM, mkalisimamie hili wabunge wote ambao hawajahudhuria kikao hiki, waandike barua za maelezo," alisema Magesa.

"Na bahati nzuri mimi ndio msimamizi wa uchaguzi ngazi ya chama na wasipohudhuria kikao kingine nitajua nini cha kufanya. Wasifanye chama kuwa lifti ya mafanikio yao," aliongeza.

Wabunge waliohudhuria kikao hicho ni Eliai Kwandikwa (Ushetu), Ezikiel Maige (Msalala)na Azza Hilal wa Viti Maalum.

Wabunge ambao hawakuhudhulia ni Stephen Masele (Shinyanga Mjini), Ahmed Salum (Solwa), Jumanne Kishimba (Kahama Mjini), Suleiman Nchambi (Kishapu) na Lucy Mayenga (Viti Maalum).

Kwa upande wake, Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Zainab Telack, akisoma taarifa ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM, alisema imetekelezwa kwa kiwango kikubwa zikiwamo sekta za kilimo, elimu, afya, maji, viwanda, ardhi, madini, nishati na barabara.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein akifungua mkutano wa Mawaziri wa SADC, katika ukumbi wa Hoteli ya Madinat Al Bahr, Mbweni nje ya mji wa Zanzibar jana. Kushoto ni Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi na Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Hassan Khatib Hassan (katikati). **PICHA: IKULU ZANZIBAR**

# Shein ataka mipango imara kupambana na maafa SADC

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, ameitaka Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) kuwa na mipango na mikakati ya kupambana na maafa hasa yale yanayotokea mara kwa mara.

Dk. Shein aliyasema hayo jana katika hotuba yake alipokuwa akifungua mkutano wa kwanza wa Kamati ya Mawaziri wenye Dhamana ya Menejimenti ya Maafa kwa nchi wanachama wa SADC unaofanyika katika Hoteli ya Madinat Al Bahr nje kidogo ya Zanzibar.

Alisema kwa kuzingatia athari za maafa zinazogharimu maendeleo ya kiuchumi na kijamii katika nchi za SADC, ni lazima jumuiya hiyo ijipange vizuri kwa kuandaa mikakati imara ya kuvitambua na kuviwahi viashiria vipya vya maafa kila vinapoanza kujitokeza.

Dk. Shein alisema kamati hiyo ina nafasi ya kutoa maelekezo na mapendekezo juu ya nini kifanyike kwa ngazi ya kitaifa na kikanda ili kujikinga na virusi vya Corona (Covid-19) ambavyo tayari yameshaenea katika nchi mbalimbali duniani.

Aidha, alisema changamoto ya nzige iliyojitokeza hivi karibuni katika ukanda wa Afrika Mashariki, ambao wanaweza kuathiri kwa kiasi kikubwa sekta ya kilimo na usalama wa chakula katika baadhi ya nchi ni suala ambalo linahitaji kuzungumzwa na kupangiwa mikakati ya pamoja.

"Wahenga wanasema tahadhari kabla ya athari, naamini kwamba haya ni miongoni mwa majukumu ya Kamati hii inayoshughulikia na masuala ya maafa", alisisitiza Rais Dk. Shein.

Katika hotuba yake hiyo Dk. Shein alimpongeza Rais John Pombe Magufuli ambaye ni Mwenyekiti wa Jumuiya ya SADC kwa kuendelea kuiongoza vyema Jumuiya hiyo hatua ambayo imepelekea kupata mafanikio makubwa sambamba na kuiletea maendeleo endelevu Tanzania.

Dk. Shein alisema kufanyika kwa mkutano huo ni hatua muhimu katika kujenga matumaini mapya ya wananchi kuhusiana na maafa, kuzingatia kwamba miaka ya hivi karibuni kumekuwa na ongezeko kubwa la maafa pamoja na viashiria vyake katika nchi wanachama wa SADC.

Shein aliongeza kuwa maafa hayo husababisha upotevu wa maisha, mali za watu na uharibifu wa miundombinu na hivyo yanaathiri sana ajenda za maendeleo zinazopangwa kutekelezwa na nchi wanachama wa SADC.

Rais Dk. Shein alieleza kuvutiwa na ajenda kuu ya mkutano huo yenye kaulimbiu "Ushiriki wa Kisekta katika Kupunguza Madhara ya Maafa ni Njia Bora ya Kujenga Uhilimi katika Ukanda wa SADC".

HABARI KITAIFA

# Waziri ahamasisha ufugaji nyuki

**Na Lusungu Helela**

NAIBU Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu (pichani chini), amehamasisha wakazi wa kisiwa cha Ukerewe mkoani Mwanza kufuga nyuki kutokana na faida ya asali kiuchumi na kiafya.

Pia Kanyasu ametoa ruhusa kwa wananchi wenye nia ya kufuga nyuki kuitumia misitu ya hifadhi mitano iliyoko katika kisiwa hicho inayosimamiwa na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya hiyo.

Kanyasu alitoa ruhusa hiyo kutokana idadi kubwa ya watu katika kisiwa hicho huku kukiwa na ufinyu wa ardhi.

Alisema lengo la kutoa hamasa na ruhusa hiyo ni kuwasaidia wananchi kubadili mfumo wa maisha kwa kuanza kufuga nyuki kibiashara badala ya kulima na kuvua samaki pekee.

Akizungumza juzi na kikundi cha watu wenye ulemavu wanaojishughulisha na useremala wa kutengeneza mizinga ya nyuki ya kisasa mjini Nansio, Naibu Waziri alisema misitu hiyo mitano yenye hekta 1,300 itawasaidia kuitumia kufuga nyuki kibiashara.

Naibu Waziri alisema kutokana na ongezeko kubwa la watu katika kisiwa hicho chenye mita za mraba 700 ambao sasa wanakadiriwa kufikia 400,000 wakazi hao wana kila sababu ya kujiingiza kufuga nyuki.

Aliwaambia wananchi hao kuwa kutokana na ardhi ya kilimo kuchoka pamoja na kupungua kwa samaki kutokana na kukithiri kwa uvuvi haramu, njia mbadala ni kufuga nyuki kutokana na mahitaji makubwa ya asali ndani na nje ya nchi.

Kanyasu aliwahakikishia uwapo wa soko la uhakika kutokana na mahitaji makubwa ya asali China na Marekani.

Alisema Tanzania bado haijakidhi mahitaji ya soko hilo.

Kwa mujibu wa Kanyasu, China pekee inahitaji tani 600,000 za asali lakini kutokana na uzalishaji duni, Tanzania bado haijasafirisha hata nusu tani ya asali inayohitajika.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe, Esther Chaula, ameahidi kutoa mkopo kwa kikundi hicho cha watu wenye ulemavu ili watengeneze mizinga mingi itakayowezesha upatikanaji wa kutosha kwa ajili ya kufugia nyuki.

Alisema ufugaji wa nyuki katika misitu hiyo ya TFS utatoa ahueni ya ulinzi shirikishi kwa vile wananchi wataona faida ya moja kwa moja kupitia asali wanayoipata.

Katika hatua nyingine, Kanyasu aliiagiza TFS kuhakikisha inanunua mavazi maalum ya kurinia asali na kuyasambaza katika vituo ambayo wananchi watakuwa wakiyaazima wakati wa kurina asali badala ya kuendelea kutumia moto wakati wa kurina.

Alisema takribani nyuki bilioni moja kila mwaka huuawa kwa moto kutokana na urinaji huo ambao si rafiki wa mazingira.



# Serikali yajivunia ongezeko la wanawake katika uongozi

**Na Joseph Mwendapole**

SERIKALI imesema inajivunia ongezeko la wanawake kwenye nafasi za uongozi ikitolea mfano wa majaji wanawake ambao wameongezeka kutoka 24 mwaka 2015 hadi 40 mwaka jana.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na Msemaji wa Wizara ya Afya, maendeleo ya Jasmii, Jinsia, Wazee na Watoto, Prudence Constantine, wakati akizungumza na waandishi wa habari kwenye Chuo cha Ustawi wa Jamii (ISW).

Alikuwa akizungumzia maadhimisho ya siku ya wanawake duniani ambayo hufanyika Machi 8, kila mwaka duniani kote na kwa nchini mwaka huu zinafanyika kitaifa mkoani Simiyu.

Constantine alisema serikali imeendelea kutekeleza maazimio ya mkutano wa Beijing kwa kuweka mazingira wezeshi ya kukuza usawa wa jinsia na uwezeshaji wanawake.

Alisema serikali imeendelea kuwawezesha wanawake kiuchumi kuondoa umaskini, kutoa elimu, mafunzo na ajira, kukuza ushiriki wao kwenye nafasi za uwakilishi na ngazi za maamuzi na kuwajengea uwezo katika sheria.

Pia alisema serikali imefanikisha kuanzishwa kwa mfuko wa uwezeshaji wananchi kiuchumi pamoja na maendeleo ya wanawake wenye masharti nafuu ambao umesaidia kutoa mikopo nafuu na mafunzo ya stadi za biashara.

Alisema tangu mwaka 2015 serikali imeendelea kutoa Sh. bilioni 28.8 ambazo zimesaidia vikundi 13, 619 vya wanawake na kufanya idadi ya wanawake wajasiriamali walionufaika na fedha hizo kufikia 883,724.

Tanzania, alisema imefanya mabadiliko kwenye utoaji wa fedha za halmashauri kwaajili ya mikopo ya wanawake na marekebisho ya sheria ya fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ya 2008 uchangiaji wa mikopo umekuwa wa kisheria.

Constantine alisema Tanzania jumla ya vikundi 19,874 vya wanawake wajasiriamali vimehamasishwa na kuanzishwa kwa kipindi cha mwaka 2017/18 na kwamba serikali imewezesha wanawake wajasiriamali kushiriki biashara na maonyesho ya kimataifa.

Pia alisema serikali imeendelea kuweka mazingira rafiki ya kisheria kwa wanawake ili kuwawezesha kupata haki zao za msingi ikiwamo kuzifanyia marekebisho sheria mbalimbali na kutunga mpya kuwalinda.


BONANZA

**BONANZA TRADING COMPANY LIMITED**

**VACANCY ANNOUNCEMENT**

**Introduction**

Bonanza Trading Company Limited is a private company registered on 30th April 2014 and Licensed by Tanzania Gaming Board to run the Business of Route/ Slot Machines in Tanzania. The company's head office is in Dar es Salaam and its business has been spreading all over Tanzania for more than 50 districts.

Bonanza Trading Company Limited would like to attract additional Human Resource as follows:-

1. **Branch Manager**
   Applicant must have the following qualifications:-
   (a) Bachelor Degree of Electronics or Mechatronic engineering or related field.
   (b) Ten(10) years working experience in the same position
2. **Technical Manager**
   Applicant must have the following qualifications:-
   (a) Bachelor Degree of Electronics or Mechatronic engineering or related field
   (b) Seven(7) years working experience in the same position
3. **Slot Technician**
   (a) Bachelor Degree of Electronics or Mechatronic engineering or related field
   (b) Five(5) years working experience in the same position
4. Slot Assistant Technician
   (a) Bachelor Degree of Electronics or Mechatronic engineering or related field
   (b) Three (3) years working experience in the same position

**General conditions**

1. All nationalities are encouraged to apply but Tanzanian citizens will be given priority.
2. Applicants must attach an up to date Curriculum Vitae (CV) having reliable contacts; postal address/post code, email and telephone numbers.
3. Applicants must attach their certified copies of their certificates.
4. Attaching copies of the following certificates is strictly not accepted;
   - Form IV and form VI results slips
   - Testimonials and all partial transcripts
5. Applicants should indicate three reputable referees with their reliable contact.
6. Certificates from foreign examination bodies for Ordinary or Advanced level education should be verified by the National Examination Council of Tanzania (NECTA) and National Council for Technical Education (NACTE).
7. Certificates from Foreign Universities should be verified by the Tanzania Commission for Universities (TCU).
8. Applicants should apply on the strength of the information given in this advertisement.
9. Presentation of forged certificates and other information will necessitate to legal action.
10. A signed application letters should be written in English and addressed to:

**HUMAN RESOURCE MANAGER**
**BONANZA TRADING COMPANY LIMITED**
**P.O. Box 13959 Dar es Salaam, Tanzania**
**Plot 461 Avocado St. Kawe Low Density Area**

**Application may be delivered to the P.O Box 13959 or submit an electronic application to Email: bonanzatradingcompanyltd@yahoo.com**

11. **Deadline for application is 22nd March 2020**

12 **.Only shortlisted candidate will be informed on a date for interview.**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kufungiwa waamuzi kuende sambamba na ubovu viwanja

**WIKI** hii Ligi Kuu Bara inaingia raundi ya 23 kwa viwanja 10 nchini kuwaka moto wakati timu zote 20 zitakaposhuka dimbani leo na kesho kuwania alama tatu muhimu.

Hadi sasa katika mzungungo huu wa lala salama, zipo klabu zinazopigia hesabu ya ubingwa wakati huu mabingwa watetezi Simba wakiwa kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo na alama zao 59, huku zingine zikiwania kumaliza katika nafasi nzuri ili kuepuka na janga la kushuka daraja.

Hata hivyo, katika raundi hii ya lala salama, Bodi ya Ligi Kuu Tanzania (TPLB) inapaswa kuongeza umakini kwani ni kipindi ambacho timu nyingi hujiingiza katika vitendo vichafu vya kupanga matokeo husussan zile zilizokata tamaa ya kubaki Ligi Kuu msimu ujao.

Nipashe tunaipongeza TPLB kwa hatua ambayo imeanza kuichukua kwa kuwafungia baadhi ya waamuzi ambao wameshindwa kutafsiri vema sheria 17 za soka kwa kuzinyonga baadhi ya timu kwa kuzisababishia kushindwa kupata matokeo.

Tunatambua wapo waamuzi ambao ni kweli wanashindwa kutafsiri sheria hizo 17, lakini pia wapo wanaozifinyanga ama kwa kutokana na mapenzi yao kwa baadhi ya timu au kwa kupokea rushwa ili kutoa upendeleo.

Hivyo ndivyo ilivyo na kwa mantiki hiyo, TPLB haina budi kuwa makini ili kuhakikisha mwisho wa msimu anapatikana bingwa halali atakayekwenda kuiwakilisha vema Tanzania kwenye michuano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa.

Lakini pia tunaikumbusha TPLB kutojisahau katika suala zima la ubora wa viwanja kwani ili kupata bingwa aliyestahili ni lazima ihakikishe soka linachezwa katika viwanja bora na rafiki kwa mchezo huo. Tunatambua hivi karibuni TPLB ilivifungia baadhi ya viwanja kutokana na kukosa ubora husussan eneo la kuchezea 'pitch' na uwezo ama kutokidhi vigezo kwa uzio wa kutenganisha mashabiki na eneo la uwanja. Hata hivyo, suala la eneo la kuchezea linapaswa kutazamwa mara kwa mara na TPLB haipaswi kulala katika kuvifungia viwanja vibovu.

Nipashe kama wadau wa soka, mara zote tumekuwa tukisafiri kwenda mikoa mbalimbali nchini kuripoti mechi za Ligi Kuu na kwa ujumla hatufurahishwi na baadhi ya viwanja ukiwamo wa Ushirika mjini Moshi na ule wa Nangwanda Sijaona na hali kadhalika wa Mkwakwani jijini Tanga.

Viwanja hivi si rafiki kwa afya za wachezaji kwani maeneo makubwa kuna vipara vya nyasi na mashimo mashimo mengi ambayo hayaruhusu mpira kutembea kwa timu iliyozoea kucheza pasi za chini. Hatutaki kuona baadhi ya timu zikilazimika kuwakosa wachezaji wake katika mzunguko huu wa lala salama kutokana na kupata majeraha yaliyosababishwa na ubovu wa uwanja.


Tunatambua ukiondoa Uwanja wa Taifa na Uhuru ambavyo hutumiwa na timu za jijini Dar es Salaam na ule wa Azam Complex, Chamazi, wa Azam FC (uliopo kwenye matengenezo), Kaitaba mkoani Kagera, Samora mjini Iringa na ule wa Nyamagana jijini Mwanza kwa asilimia kubwa vilivyosalia si rafiki kwa timu kuweza kucheza soka la kueleweka la pasi za chini.

Lakini pia hatuoni sababu ya Uwanja kama wa Ushirika kutokuwa na nyasi rafiki wakati Moshi kuna maji ya kutosha, huku hali ya hewa ikiruhusu nyasi kumea vizuri.

Hivyo, tuna kila sababu kuikumbusha TPLB kuzikumbusha klabu husika ama wahusika ili kuendelea kuhudumiwa viwanja hivyo kuonekana bora kwa msimu mzima husussan eneo la kuchezea kwani mbali na kutaka kuona wachezaji wakicheza soka kwa uhakika bila hofu ya kuumia kutokana na ubovu wa uwanja, lengo letu pia ni kuona watazamaji hawajutii kutoa viingilio vyao.

Aidha , tunatambua kiasi kikubwa cha mapato ambacho wamiliki wa viwanja hivyo huingiza kutokana na kutumika katika mechi, hivyo pasipo msukumo mkubwa wa ukarabati kutoka TPLB, tunawaomba waone haja ya kuvitunza kwa msimu mzima ili kuendelea kutumika na kuwaingizia kipato.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Nyosso anapotuonyesha tatizo la mabeki Bongo



Na Adam Fungamwango

**MARA** baada ya mechi kati ya Simba dhidi ya Kagera Sugar, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Sven Vendenbroeck, alionyesha kushangazwa na uwezo mkubwa wa beki mkongwe nchini, Juma Nyosso.

Alionekana kusuuzika mno na aina yake ya uchezaji na kuona kuwa hivi ndivyo beki anavyotakiwa kucheza baada ya kula sahani moja na John Bocco na kumpa wakati mgumu mno.

Sven, akauliza kama anaweza kumpata beki huyo kwenye kikosi chake cha Simba. Alishangaa aliposikia kuwa beki huyo alishawahi kuichezea Simba miaka kadhaa nyuma.

Kwa nini aliondoka? Hilo ni swali lingine. Kwa hali ilivyo ni kwamba wanachama na mashabiki wa Simba wasishangae kuona Nyosso akirejea tena Msimbazi kwa mara nyingine tena baada ya miaka mingi.

Nyosso alijiunga na Simba mwaka 2008, akitokea Ashanti FC na kukaa kwa miaka mitano, hadi 2013, alipohamia Coastal Union na baada ya hapo kwenda kuichezea Mbeya City, kabla ya kutua Kagera Sugar.

Bado anaonekana kuwa wamo. Pamoja na kwamba ni mchezaji wa muda mrefu, lakini bado ana nguvu, akitimiza majukumu yake yote ambayo beki anatakiwa kuyafanya.

Hata yale matatizo yake ya utovu wa nidhamu anaonekana kuwa amejirekebisha na badala yake amejikita zaidi kucheza soka.

Mwenyewe ametanabaisha kuwa hakuna straika anayemhofia Tanzania kama John Bocco na kudai ni mchezaji mwenye uwezo wa hali ya juu, nguvu, anayeweza kuwaadhibu wakati wowote ule mabeki wanapozubaa.

Tayari baadhi ya wachambuzi wa soka nchini wameshaanza kumpigia chapuo kuitwa kwenye kikosi cha timu ya Taifa, Taifa Stars kitakachoenda kucheza michuano ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani, CHAN.

Itakumbukwa pia kuwa mara baada ya Fainali za Afrika (Afcon), mabeki wakongwe nchini, Kelvin Yondani na Erasto Nyoni walitaka kutangaza kujiuzulu kuichezea timu ya taifa.

Hata hivyo, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda aliwataka wasitishe mpango huo mara moja na kuwaomba waendelee kuichezea timu hiyo, si kwa manufaa yao tu, bali hata kwa taifa zima. Na hii ndiyo imefanya hadi leo wachezaji hao wawe kwenye kikosi cha timu ya taifa.

Makonda naye ni mwanasoka, aliona kabisa kama mabeki hawa wakijiuzulu, basi eneo la ulinzi kwenye kikosi cha Stars litakuwa matatizoni.

Ni kweli kabisa alikuwa sahihi. Kwa muda mrefu sasa nchini Tanzania kuna uhaba, au matatizo makubwa kwa wachezaji wa safu ya ulinzi hasa kwa wachezaji vijana.

Kile kizazi cha mabeki wenye nguvu, ambao pia wanatumia akili kimeanza kuondoka, na waliobaki ndiyo hawa kina Nyosso, Nyoni ,Yondani au Aggrey Morris wanaishia, badala yake sasa huko mbele ya safari tunaweza kuona mabeki wengi wakitoka nje ya nchi.

Mabeki wengi wa kisasa, hawana nguvu, badala yake wanaona kucheza ubabe ndiyo nguvu au rafu nyingi zisizo na maana, lakini pia hawana muendelezo wa uwezo wao, leo wanaweza kucheza vizuri, kesho matatizo, tofauti na mabeki hawa wakongwe niliowataja ambao wameanza kujulikana tangu katikati ya miaka ya 2000, hadi leo wapo dimbani.

Beki pekee kijana ambaye Tanzania inajivunia kwa sasa anayefuata nyayo za kaka zake hao, ni Bakari Mwamnyeto.

Ni kijana mwenye sifa zote zinazohitajika kuwa beki bora, akicheza kwa kiwango kikubwa akiwa na Coastal Union kwenye mechi zote, lakini hata timu ya taifa pia, amekuwa na kiwango kile kile kama cha kwenye timu yake.

Waliobaki ni wa kawaida tu, wengine wakiwa na viwango vya kupanda na kushuka na homa za vipindi.

Unapoona hadi kocha mgeni wa Simba, pamoja na timu yake kucheza mechi kadhaa za Ligi Kuu na FA, lakini akakunwa na beki mmoja tu, Nyosso ambaye ni mkongwe, huku pia mashabiki wa soka akiwamo Mkuu wa Mkoa, Makonda kuwataka Nyoni na Yondani waendelee kuichezea timu ya taifa, ujue kuna matatizo kwa mabeki wa kizazi cha sasa nchini.

Nilitegemea kwa sasa kuwapo kwa mabeki wengi bora wanaochipukia na kuwafanya kina Nyosso kufikiria kutundika daluga, lakini wapi. Sijui mabeki vijana wanaochipukia wa Kibongo wanakwama wapi?

HABARI KITAIFA

# Mtatiro awaonya viongozi ushirika

**Na Gideon Mwakanosya,**
TUNDURU

MKUU wa Wilaya ya Tunduru, Julius Mtatiro, amevitaka vyama vya akiba na mikopo (Saccos) kuzingatia taratibu na sheria katika uendeshaji wa kazi zao na kuacha kufanya mambo kwa mazoea ili kuepusha vyama hivyo kufa.

Mtatiro alitoa kauli hiyo jana alipokuwa akifungua mafunzo ya siku tatu ya vyama vya akiba na mikopo yaliyoandaliwa na mrajisi msaidizi wa vyama vya ushirika mkoa wa Ruvuma kwa kushirikiana na Tume ya Maendeleo ya Ushirika, Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (Coasco), Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi na maofisa ushirika wa wilaya ya Tunduru.

Pia aliwaonya viongozi hao kuacha mchezo mchafu na vitendo visivyokubalika na kuwataka wana ushirika wote kuwa ma msimamo wa kujali wakulima na ukuaji wa vyama vya ushirika.

Aidha, aliwakumbusha viongozi hao serikali ya wilaya iko macho na itahakikisha wale wote wanaotaka kujaribu kuyumbisha ushirika katika uchaguzi unaoendelea watachukuliwa hatua za kisheria.

Sambamba na hilo, aliwataka kuuchukulia ushirika kama sekta muhimu na yenye tija huku akitolea mfano kuwa Tunduru katika msimu wa mwaka 2018/19, wakulima walipata Sh. bilioni 61 kutokana na korosho.

Alisema katika msimu 2019/20, wakulima wa Tunduru walipata Sh. bilioni 67 huku wakitarajia kupata zaidi ya Sh. bilioni tano kutokana na ufuta.

Mtatiro alisisitiza kuwa fedha zote hizo zinapitia katika vyama vya msingi vya ushirika na akawataka wadau wa vyama hivyo kuhakikisha wanachagua viongozi wenye uwezo na wanaolinda na kutetea maslahi na fedha za wakulima.



Mkuu wa Kitengo cha Mauzo, Usambazaji, Maduka na Huduma kwa Wateja Vodacom Tanzania Plc, George Lugata (kulia), akikata utepe kuzindua duka jipya la Vodacom Mbezi Beach chini kwa Zena, jijini Dar es Salaam jana. Kushoto kwake ni Msimamizi wa duka hilo, Devota Kijogoo na wafanyakazi wa kampuni hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wapewa somo kuhusu kulipa kodi

**Na Robert Temalilwa**

WATANZANIA wametakiwa kumuunga mkono Rais John Magufuli katika kuendelea kuiletea nchi maendeleo kwa kuhakikisha kila mmoja anatimiza wajibu wa kulipa kodi kwa wakati na ipasavyo.

Wito huo ulitolewa juzi jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi wa Shirika lisilo kiserikali la Sema na Rais Wako (SRW), Mohamed Mkindi, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusiana na kazi kubwa inayofanywa na serikali ya awamu ya tano chini ya Rais Magufuli.

Mkindi alisema kila Mtanzania anayepaswa kulipa kodi na akilipa ipasavyo ni wazi nchi itaendelea kupiga hatua kubwa kimaendeleo.

"Niwaombe Watanzania wenzangu tuunge mkono juhudi za Rais wetu kwa kuhakikisha tunalipa kodi kwa wakati ili zisaidie kutuletea maendeleo," alisema Mkindi.

Alisema maendeleo yanapatikana kwa ukusanyaji mzuri wa mapato, hivyo ni vyema elimu ikaendelea kutolewa kwa ajili ya ulipaji kodi.

Mkindi aliongeza kwa kuwataka viongozi wa vyama vya siasa kuacha kubeza kila jambo la maendeleo linalofanywa na serikali huku akisisitiza kuwa maendeleo yanayofanywa na serikali ni kwa ajili ya Watanzania wote na si kwa faida ya CCM tu.

"Tusipelekwe vibaya na siasa bali penye ukweli tuseme ukweli. Chama chochote cha siasa lengo kuu ni kushika dola, hivyo pindi wapinzani watakapochukua nchi watakuta nchi tayari ina maendeleo, hivyo si vyema kubeza kila kitu kinachofanywa na serikali," alisema.

Aidha, aliwataka vijana wanaodai kukosa pesa mfukoni kuhakikisha wanafanya kazi kwa bidii badala ya kushinda vijiweni huku wakitegemea 'miujiza' ya kupata pesa.

"Vijana wenzangu tuache kulalamika kuwa hatuna fedha mfukoni wakati kazi hatutaki kufanya. tufanye kazi kwa bidii ili kupata pesa, " alisema.

# Nondo ajitosa uongozi ACT

**Na Enock Charles**

MWANACHAMA wa Chama cha ACT-Wazalendo na aliyekuwa Mwenyekiti wa Mtandao wa Wanafunzi Tanzania (TSNP), Abdul Nondo, amechukua fomu kuwania nafasi ya Uenyekiti wa Ngome ya Vijana wa chama hicho.

Akizungumza na vyombo vya habari wakati akichukua fomu ya kuwania nafasi hiyo katika makao makuu ya chama hicho jijini Dar es Salaam jana, Nondo aliahidi kuongeza ari kwa vijana nchini kushiriki katika masuala ya kisiasa.

Alidai vijana wengi sasa wamekata tamaa kushiriki siasa na kwamba chama hicho kwa sasa kinahitaji mwenyekiti wa vijana atakayeongelea matatizo ya vijana, hasa ukosefu wa ajira nchini.

"Tunahitaji Mwenyekiti wa Ngome ya Vijana ambaye yupo tayari kutetea maslahi ya vijana na pia kulinda na kutetea demokrasia nchini," alitamba.

Alisema ngome hiyo itapambana kulinda chama hicho ikiwa ni pamoja na kupambana na hujuma mbalimbali zinazofanyika kuhujumu viongozi wakuu wa chama hicho Tanzania Bara na Zanzibar kama vile vitisho vinavyotolewa kwa dhidi ya viongozi hao.

Nondo aliwahi kushitakiwa na serikali miaka miwili iliyopita alipoonekana Mafinga mkoani Iringa baada ya kuripotiwa kutekwa na watu wasiojulikana aliodai walimsafirisha kutoka Dar es Salaam hadi mkoani Iringa wakati huo akiwa ni mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Mwenyekiti wa mtandao wa Wanafunzi Tanzania.

Novemba 5 mwaka 2018, Mahakama ya Hakimu Mkazi Iringa ilimwachia huru Nondo kutokana na Upande wa Jamhuri kushindwa kuthibitisha mashitaka mawili aliyoshitakiwa nayo, moja likiwa ni kuchapisha taarifa za uongo mtandaoni na

# Kortini tuhuma za rushwa ya mil. 16/-

**Na Hellen Mwango**

MFANYABIASHARA Perpetua Gondwe amefikishwa mahakamani akikabiliwa na mashtaka matano ikiwamo kujipatia rushwa ya zaidi ya Sh. milioni 16 kwa lengo la kumtoa Edger Fuluga aliyekuwa anashikiliwa katika Kituo Kikuu cha Polisi jijini Dar es Salaam.

Gondwe alifikishwa na kusomewa mashitaka katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Rashid Chaungu.

Mwendesha Mashtaka wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Domonic Prudence, alidai kuwa Januari 18, mwaka huu katika Kituo Kikuu cha Polisi jijini Dar es Saalam, mshitakiwa huyo alijipatia Sh. milioni 3.5 kutoka kwa Scholastica Minja kwa niaba ya askari polisi, Konstebo Wilbard Msaki, ili amwachie Fuluga aliyekuwa anashikiliwa katika kituo hicho.

Katika shtaka la pili, ilidaiwa kuwa Januari 19, mwaka huu, katika kituo hicho cha polisi, mshtakiwa alijipatia Sh. milioni mbili kutoka kwa Minja kwa niaba ya Msaki ili amwachie mtuhumiwa wa uhalifu Fuluga.

Shtaka la tatu, ilidaiwa kuwa tarehe hiyo hiyo na katika kituo hicho cha polisi, mshtakiwa alijipatia Sh. milioni mbili kutoka kwa Minja kwa niaba ya Msaki ili amwachie mtuhumiwa huyo.

Katika shtaka la nne, ilidaiwa Januari 20, mwaka huu, Gondwe alijipatia Sh. milioni 4.5 kutoka kwa Minja kwa niaba ya Msaki ili amwachie Fuluga.

Upande huo wa Jamhuri ulidai katika shtaka la tano, mshtakiwa alijipatia Sh. milioni mbili kutoka kwa Minja kwa niaba ya Msaki ambaye ni mwajiliwa wa Jeshi la Polisi ili amwachie mtuhumiwa.

Mshitakiwa alikana mashtaka hayo na upande wa mashtaka ulidai kuwa upelelezi wa shauri hilo bado haujakamilika, hivyo kuomba tarehe nyingine ya kutajwa.

Hakimu Chaungu alisema dhamana iko wazi kwa mshtakiwa huyo, hivyo anatakiwa kuwa na mdhamini mmoja atakayetia saini hati ya dhamana ya Sh. milioni 15.

Gondwe aliachiwa kwa dhamana baada ya kutimiza masharti na kesi imepangwa kutajwa Machi 18, mwaka huu.




Wanafunzi wa shule mbalimbali za msingi na sekondari wa Mkoa wa Rukwa, wakiwa wamebeba mabango yenye ujumbe mbalimbali za kupinga ukatili wa kijinsia, wakati wa uzinduzi wa Mpango Mkakati wa Kukabiliana na Matukio ya Mimba Shuleni, katika Mji wa Namanyele, Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi, juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# RC Hapi ahimiza ulipaji kodi kwa hiari

**Na Mwandishi Wetu**

MKUU wa Mkoa wa Iringa, Ally Hapi, amewataka wafanyabiashara nchini kuwa na mazoea ya kulipa kodi kwa wakati na hiari, akieleza kuwa kufanya hivyo kutasaidia Ukuaji wa uchumi na maendeleo ya nchi.

Alitoa rai hiyo jana alipotembelewa na timu ya maofisa wa Mamlaka ya Mapato (TRA) ambayo iko mkoani humo kufanya kampeni ya elimu kwa mlipakodi.

Hapi alisema hatua ya wafanyabiashara kulipa kodi kwa hiari ni jambo la ufahari na uzalendo.

"Wito wangu kwa wafanyabiashara wa Mkoa wa Iringa na maeneo mengine ni kwamba, kila mfanyabiashara afahamu kulipa kodi ni jambo la fahari na uzalendo, hivyo ni wajibu wa kila mfanyabiashara kuhakikisha analipa kodi kwa wakati ili kusaidia maendeleo ya nchi yetu na sekta mbalimbali ambazo zinategemea kodi katika kujiendesha," alisema.

Vilevile, aliwahimiza wafanyabiashara kutembelea ofisi za TRA zilizo karibu na maeneo yao kwa ajili ya kupata uelewa na ushauri wa masuala mbalimbali ya kikodi ambayo yatawasaidia wasifanye makosa.

"Mamlaka yetu sasa imepanua huduma zake zaidi, kwa wale wafanyabiashara ambao wanatatizwa na masuala ya kikodi, nitumie fursa hii kutoa wito kwao kwamba, tunazo ofisi za Mamlaka ya Mapato katika wilaya zetu zote, wafike kwa ajili ya kuuliza, kupata uelewa na pengine kupata ushauri ambao utawasaidia wasiingie katika makosa ya kikodi.

"Tunatamani kuwa na wafanyabiashara wanaofanya shughuli zao vizuri, lakini pia pale wanapopata mkwamo wa aina yoyote, wasisite kuwasiliana na Mamlaka ya Mapato katika maeneo yao ili kuhakikisha kuwa wanapata ushauri sahihi," alisema.

Alisema kuwa kila mfanyabiashara ana mchango katika maendeleo yanayopatikana ndani ya taifa hili, hivyo ni muhimu watu wawe na utamaduni wa kulipa kodi ili serikali itekeleze majukumu yake na wao wawe na haki ya kudai na kuona fahari juu ya maendeleo yanayofanyika nchini.

Kiongozi wa timu ya maofisa wa TRA wanaofanya kampeni ya elimu kwa mlipakodi mkoani humo, Rose Mahendeka, alimweleza Mkuu wa Mkoa huo kuwa, tayari timu hiyo imeshawafikia wafanyabiashara takribani 600 katika Wilaya ya Kilolo na inaendelea na kampeni katika Wilaya ya Iringa mjini na Mufindi.

Timu ya elimu kwa mlipakodi inapita mlango kwa mlango katika maduka ya wafanyabiashara, ikielimisha wafanyabiashara juu ya masuala mbalimbali yanayohusu kodi na kuwakumbusha kulipa kodi kwa hiari na wakati.

# Ataka wazawa kuchangamkia fursa ununuzi madini almasi

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKUU wa Mkoa wa Shinyanga, Zainab Telack, amefungua milango kwa wazawa kwenda kununua madini ya almasi kwa njia ya mnada asilimia tano ambayo huzalishwa na mgodi wa Mwadui ulioko wilayani Kishapu mkoani hapa.

Telack alibainisha hayo jana wakati wa kutangazwa washindi wanne ambao wamekidhi vigezo vya kununua madini hayo kwenye mgodi huo.

Alisema serikali kwa kushirikiana na Wizara ya Madini na Tume ya Madini, wanawakaribisha Watanzania wote kwenda kununua almasi kwenye mgodi huo ili kuinuka kiuchumi.

"Zabuni ya kununua madini haya katika mgodi huu wa Mwadui ilianza Februari 17 na leo (jana) tunatangaza washindi waliokidhi vigezo kununua," alisema Telack.

"Pia natoa wito kwa wanunuzi hawa wadogo ambao mmeshinda kununua almasi ya Mwadui mkauze kwenye masoko yetu ya madini pamoja na kulipa kodi ya serikali," aliongeza.

Aidha, alisema kabla ya kutoanzisha kwa masoko hayo ya madini serikali ilikuwa ikikusanya Sh. milioni 500 lakini baada ya masoko hayo inakusanya Sh. bilioni 10.

Naye Meneja Biashara na Mthamini wa Madini kutoka Tume ya Madini, George Kaseza, akitangaza washindi hao wa ununuzi wa almasi, alisema washindi hao kiutaratibu hawapaswi kutangazwa bali watapigiwa simu na kupewa utaratibu, huku akisema jambo hilo ni endelevu na wanunuzi wajitokeze zaidi

Katibu wa Wanunuzi wa Almasi wilayani Kishapu, Masanja Meja, aliipongeza serikali kwa kuwajali wazawa kunufaika na rasilimali za nyumbani, huku akiomba kwenye ununuzi wa madini hayo ya Mwadui, kodi iondolewe ili wanufaike zaidi.



# HABARI ARUSHA




Mwenyekiti wa Taifa wa Jumuiya ya Wazazi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Edmond Mndolwa (kushoto), akizungumza kabla ya kukabidhi mashine ya kufyatua matofali kwa jumuiya hiyo, Wilaya ya Longido, akiwa katika ziara ya kukagua utekelezaji wa ilani ya chama hicho, mkoani Arusha jana. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

## Wakazi kata za pembezoni wakumbukwa huduma afya

**Na Allan Isack,** ARUMERU

SHIRIKA lisilo la kiserikali la Aspiration for Vulnerable Rehabiltated Families (Avurefa), limeanzisha mpango wa kutoa huduma za afya za mkoba katika kata za pembezoni katika Halmashauri ya Arusha, wilayani Arumeru.

Imeelezwa kuwa lengo la kuanzishwa kwa huduma hiyo ni kupambana na magonjwa sugu na kutoa huduma bora kwa wagonjwa.

Akizungumza wakati wa kulitambulisha shirika hilo kwenye kikao kazi wilayani humo, Mkurugenzi wa Shirika la Avurefa, Dk. Furaha Kitiwe, alisema shirika hilo limeweka mpango wa kutoa huduma za afya za majumbani katika maeneo ya kata za pembezoni ili kuwahudumia wagonjwa waathirika wa Virusi vya Ukimwi (VVU) na kifua kikuu, utapiamlo, huduma za afya ya uzazi na uzazi wa mpango.

"Tutashirikiana na halmashauri kutoa huduma hizo kupitia utaratibu wa mkoba kwa kuwafikia watu katika maeneo yao. Lengo ni kutoa elimu ya kujikinga na maambukizo ya ugonjwa wa Ukimwi, kifua kikuu, kansa ya mlango wa kizazi na kutambua dalili za awali, kupima, kutibu na kuzuia maambukizo," alisema.

Dk. Kitili alisema shirika hilo litashirikiana na wataalamu wa afya wa halmashauri hiyo, kuwafikia wagonjwa nyumbani kwa kutoa elimu ya maambukizo ya ugonjwa wa kifua kikuu. Alisema wataangalia dalili za ugonjwa huo na kuangalia njia za kujikinga kwa kuwafanyia vipimo, kutoa dawa na kutoa mwongozo wa kuwatunza wagonjwa hao bila ya kuwanyanyapaa. Alisema watatoa elimu ya maambukizo mapya ya VVU pamoja na kuwapa elimu ya lishe bora kwa wagonjwa.

Kitiwe alisema shirika hilo limeamua kutoa huduma hizo kwa lengo la kuunga mkono juhudi za serikali kutoa huduma bora za afya kwa wananchi hususani wa vijijini.

Akizungumza kwa niaba ya Mganga Mkuu wa Wilaya, Ofisa Afya wa Halmashauri ya Arusha, Issa Msumari, alisema halmashauri hiyo, itashirikiana na shirika hilo, kuwahudumia wagonjwa hao na kutekeleza mkakati wa serikali wa kuwafikia wagonjwa waishio maeneo ya pembezoni mwa kata na vijiji. Ofisa Mtendaji wa Kata ya Sambasha, Nkini, alisema kwenye kata hiyo, kuna uhitaji wa huduma za afya, kutokana na uelewa mdogo wa jamii kuhusu ugonjwa wa kifua kikuu na maambukizo na namna ya kujikinga na ugonjwa wa Ukimwi na namna ya kuwahudumia wagonjwa hao kwa kuwapa lishe bora.

"Bado jamii haina uelewa wa kutosha kuhusu maambukizo ya ugonjwa wa Ukimwi, ugonjwa wa kifua kikuu na namna ya kuwahudumia wagonjwa," alisema.

Shirika hilo limeanza kutekeleza mradi huo wa awali kwa kipindi cha miezi sita kwenye Kata ya Sambasha na baada ya hapo litakwenda kwenye kata zingine za pembezoni mwa halmashauri hiyo.

## Wawajengea shule 306 wanaosoma chini ya miti

**Na Allan Isack,** SIMANJIRO

WANAFUNZI 306 wa shule za awali, darasa la kwanza na la pili kwenye shule shikizi ya Mazinde, Kata ya Loiborsoit wilayani Simanjiro mkoani Manyara, wameondokana na adha ya kusoma chini ya miti baada ya kujengewa madarasa na shirika la ECLAT Foundation.

Kabla ya ujenzi wa madarasa hayo, wanafunzi wa shule hiyo walikuwa wakisomea chini ya miti.

Shirika hilo limejenga madarasa manne, matundu 16 ya vyoo na ofisi ya walimu kwenye shule hiyo.

Pia, baadhi ya wanafunzi wa eneo hilo wanatembea umbali zaidi ya kilomita 17 kwenda Shule za Msingi Loiborsoit A na Ruvu Remit kwenda kusoma.

Mwenyekiti wa ECLAT Foundation, Peter Toima, akizungumza jana wakati akikabidhi shule hiyo kwa Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, Zephania Chaula, alisema wamejenga shule hiyo baada ya kupokea maombi kutoka kwa uongozi wa kijiji.

Toima alisema shirika la ECLAT Foundation kwa kushirikiana na Taasisi ya Upendo ya Ujerumani wamejenga madarasa manne, matundu 16 ya vyoo na ofisi mbili za walimu.

"Katika ujenzi wa madarasa manne, wananchi walianza kujenga mawili, lakini hayakukamilika, hivyo taasisi yetu iliyamalizia kwa gharama zilizobakia," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, Zephania Chaula, ameupongeza uongozi wa ECLAT Foundation kwa kufanikisha ujenzi huo kwa kuwa utapunguza adha kwa wanafunzi wa eneo hilo kutembelea umbali mrefu wakati wa kwenda shuleni na kurudi nyumbani.

Alitoa onyo kwa baadhi ya wanasiasa wa wilaya hiyo wanaozusha maneno ya uongo dhidi ya shirika hilo kuwa wameingia makubaliano na halmashauri ya wilaya hiyo.

"Wanasiasa uchwara waache maneno ya uzushi, nitawachukulia hatua kali kama mtu anataka kusifiwa, basi afanye mambo ya kimaendeleo kwenye jamii tutamsifia na sisi kama serikali hatutakubaliana na maneno ya kichochezi yasiyokuwa na maana," alisema.

Ofisa Elimu ya Msingi wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro, Silvanus Tairo, alisema shule hiyo itasajiliwa hivi karibuni na itaitwa Shule ya Msingi Mazinde.

Mwalimu wa shule hiyo, Kaika Elias, alisema alikuwa akifundisha peke yake wanafunzi 306 kwa kuwa mwalimu aliyekuwa akisaidiana naye alihama eneo hilo. Alishukuru shirika hilo kwa kujenga shule hiyo kwa kuwa wanafunzi walikuwa wakitembea umbali mrefu kwenda kusoma shule za jirani.

## Waona shida fikra bidhaa za ndani

**Na Allan Isack,** ARUMERU

WADAU wa sekta ya mifugo katika Halmashauri ya Arusha wilayani Arumeru, wameitaka jamii kuachana na dhana potofu ya kuthamini bidhaa zinatoka nje ya nchi kuwa ni bora kuliko zile zinazozalishwa nchini.

Wakizungumza katika hafla fupi ya kuwakabidhi vyeti iliyofanyika jijini Arusha, walisema tatizo linalowakabili wawekezaji wa sekta ya mifugo ni uelewa duni kwa jamii kuhusu mtumizi ya bidhaa za ndani.

Wadau hao wameitaka jamii kuwa na utaratibu wa kuthamini na kutumia bidhaa zinazozalishwa kwenye viwanda vya nyumbani, ili kuunga mkono jitihada za serikali ya kufikia malengo ya kufikia uchumi wa kati na wa viwanda.

Waliiomba jamii kuondokana na dhana ya kwamba bidhaa zinazotengenezwa nje ya nchi ni bora kuliko zinazozalishwa hapa nchini. Baraka Laizer, mmoja wa wadau hao, alisema wafugaji wengi wameanza kuhamasika kufuga kibiashara zaidi kwa kutumia malighafi za mifugo na kuanzisha viwanda.

Laizer alisema tatizo linalowakabili ni ushindani mkubwa wa bidhaa kutoka za nje ya nchi kutokana na dhana iliyojengeka kwenye jamii ya kutokununua bidhaa za ndani kwa kigezo cha bidhaa hizo hazina ubora.

Msimamizi wa Kiwanda cha Uchakataji Nyama cha Maasai Exports Butchery, Frenk Mollel, alisema kiwanda hicho huzalisha bidhaa za nyama zenye ubora wa kimataifa, lakini bado wananchi hawatumii bidhaa hizo kwa wingi, hivyo kusuasua katika soko la ndani.

"Watu kutoka mataifa ya nje wananunua ng'ombe nchini, wanasafirisha nje ya nchi, na huko wanatumia mashine kama tunazotumia sisi, lakini wakiingiza bidhaa hizo nchini, Watanzania wananunua bidhaa hizo kwa wingi na kwa bei kubwa wakidhani ni bora kuliko bidhaa zetu ilhali viwango vya ubora vinafanana," alilalamika.

Aliishauri serikali na taasisi zake kuwa mfano kwa kutumia bidhaa za ndani, ikiwamo nyama inayozalishwa nchini na kwa kufanya hivyo, kutawapa hamasa zaidi wananchi kutumia bidhaa zinazotengenezwa ndani ya nchi.

Leah Sangawe, mfugaji wa ng'ombe, alisema ufugaji ni zaidi ya biashara kwa kuwa ana uwezo wa kutoa malighafi nyingi za mifugo kuzalisha chakula, mavazi, dawa na mapambo.

Alitoa rai kwa wafugaji kutokukatishwa tamaa na tatizo la masoko badala yake waendelee kuzalisha bidhaa zenye ubora na ushindani katika soko la kimataifa.





Mjasiriamali Nusura Mwandinda wa Manispaa ya Moshi, akitengeneza mavazi na bidhaa mbalimbali kwa kutumia malighafi ya batiki na vitenge kwa ajili ya kuwauzia watalii mbalimbali wanaofika katika manispaa hiyo, mkoani Kilimanjaro, kwa shughuli mbalimbali za kitalii ikiwemo kupanda Mlima Kilimanjaro. **PICHA: JAMES LANKA**

# Mghwira ashtukia upigaji ujenzi barabara

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MKUU wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira, amesema anaona upungufu katika fedha nyingi zinazotumika kujenga vipande vifupi vya barabara za kiwango cha lami na kushauri fungu hilo ni bora lielekezwe kujenga barabara za changarawe vijijini.

Ushauri huo aliutoa jana, alipokuwa akizungumza na Mratibu wa Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (Tarura) Mkoa wa Kilimanjaro, Mhandisi Meleck Slaa, baada ya kufanya ziara ya kushtukiza ya kukagua barabara zinazounganisha vijiji vya pembezoni vinavyopakana na Manispaa ya Moshi ili kujiridhisha kama zinapitika kwa urahisi.

Alisema fedha nyingi zinatumika kukarabati barabara za lami za mijini lakini zinaharibika muda mfupi baadae, wakati zingeelekezwa kujenga barabara za changarawe, zingetosha kujenga kilomita nyingi za barabara hizo na makalavati.

"Mhandisi wangu mimi ninafikiri hebu tusaidieni kuhakikisha barabara zote ndani ya mkoa zinapitika kirahisi.

Ni vyema Tarura mkaweka mkazo kwenye ujenzi na matengenezo ya maeneo korofi ili wananchi waweze kufikisha bidhaa zao sokoni pamoja na kuzifikia huduma muhimu za kijamii, alisema Dk. Mghwila na kuongeza

"Najua fedha nyingi zinazotumika kujenga vipande vifupi vya barabara kwa kiwango cha lami zingetosha kujenga kilomita nyingi za barabara za changarawe pamoja na makalavati na hatimaye barabara zote zingepitika kwa urahisi zaidi."

Alisema serikali imekuwa ikitoa fedha kwa ajili ya miundombinu ya barabara lakini baadhi haikamiliki kwa wakati.

Kutokana na maelekezo hayo, Mhandisi Slaa, alimuahidi Mkuu huyo wa mkoa kwamba amepokea agizo lake na atazingatia na kutekeleza agizo hilo.

# TaCRI yazinduka kupaa bei ya kahawa

**Na Godfrey Mushi,** HAI

KUPANDA Kwa bei ya kahawa iliyoongezwa thamani katika masoko mbalimbali, sasa kumeiamsha usingizini Taasisi ya Utafiti wa Kahawa Tanzania (TaCRI), kuja na mradi mpya wa kuchochea mnyororo wa ongezeko la thamani.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi Mkuu wa TaCRI, Dk. Deusdedit Kilambo, kilogramu moja ya kahawa ya daraja la chini iliyoongezwa thamani sasa itampatia mkulima zaidi ya Sh. 4,900.

Alisema kwa kahawa ambayo haijaongezwa thamani, inauzwa sokoni kati ya Sh. 1,000 hadi Sh. 2,000. "Tunataka hivi sasa kuboresha maisha ya wakulima wa kahawa na kuwapunguzia umaskini kwa kuwapa elimu kupitia mradi wetu mpya wa ongezeko la mnyororo wa thamani," alisema Dk. Kilambo

Alisema baada ya mafanikio makubwa ya kutatua matatizo ya uzalishaji kutoka aina 19 za kahawa ya Arabika na nne za Robusta zenye tija na ubora unaokubalika katika soko la ndani na nje ya nchi, taasisi hiyo imeanza kuangalia mnyororo wa thamani wa zao hilo kutoka shambani hadi sokoni. Dk. Kilambo aliongeza kuwa wamefikia uamuzi huo baada ya kufanyika utafiti ambao ndio uhai wa wakulima na sekta na zao la kahawa Tanzania.

TaCRI imekuwa ikifanya kazi kwa kufuata mikakati ya utekelezaji ya miaka mitano mitano (SAP).

Mikakati hiyo imekuwa ikiandaliwa na wataalamu washauri kwa kutumia njia shirikishi na hasa kushirikisha wadau wa kahawa katika ngazi mbalimbali ili kufanikisha juhudi za kuongeza mnyororo wa thamani wa zao hilo.

Hivi karibuni, Wizara ya Kilimo ilisema inakusudia kuinua uzalishaji wa mazao yote ya biashara ikiwamo kahawa, baada ya kuwapunguza wakulima gharama za uzalishaji kwa kuwaondolea mzigo mkubwa wa kodi walizokuwa wakizilipa.

# Mapya yaibuka mali za mjane

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

SIKU mbili baada ya serikali ya Kijiji cha Mvuleni-Mji Mpya kilichopo Kata ya Mabogini, Wilaya ya Moshi kurejesha mali za mjane Magdalena Massao (40) alizokuwa anataka kudhulumiwa na shemeji yake, mapya yameibuka.

Mjane huyo anadai watoto wake wawili wa kike waliokuwa wameuza tofali ambazo ziliachwa na marehemu baba yao ili kutafuta ada na mahitaji mengine, wamedhulumiwa zaidi ya Sh. milioni mbili.

Akizungumzia jana madai hayo, mjane huyo alisema mpaka sasa hana uhakika ni lini watoto wake watapewa fedha hizo, ingawa baba yao mdogo ametoa 185,000 kati ya Sh. milioni mbili.

Mtoto mkubwa wa kike wa mjane huyo, Getrude Massao (24) alisema yeye ndie aliyeuza tofali za kuchoma zilizoachwa na marehemu baba yake lakini alinyang'anywa na baba yake mdogo na kupewa kiasi hicho cha fedha yeye na mdogo wake aitwaye Magreth Massao.

Kabla ya kuibuliwa kwa madai hayo, wasaidizi wa kisheria wakishirikiana na serikali ya Kijiji walifanikiwa kurejesha mali za mjane huyo ambazo ni kiwanja chenye nyumba ambayo pia haijamalizika kujengwa.

Kazi ya kuinusuru familia hiyo ilifanywa wiki moja iliyopita na wajumbe wa serikali ya kijiji hicho walioagizwa na Mwenyekiti wa Kijiji, Joseph Meza, pamoja na msaidizi wa kisheria wa eneo hilo Michael Shayo.

Ndugu wa mume wa mjane huyo, akiwamo shemeji yake (jina limehifadhiwa) alitoa amri ya kubomolewa makazi yao na kisha kuchukua mali zilizokuwa ndani ya nyumba hiyo.

Kwa mujibu wa uongozi wa kijiji hicho, anayetuhumiwa kutaka kudhulumu mali za familia ya mjane huyo hakuwa msimamizi wa mirathi.

Msaidizi wa kisheria, Michael Shayo, aliyefanikisha kurejeshwa kwa mali za mjane huyo alisema baada ya kuchunguza kwa makini na kufuatilia malalamiko ya familia hiyo uongozi wa kijiji pamoja na yeye walilitwaa eneo hilo na kulirejesha kwa mjane huyo.



# Jafo aagiza tathmini ya madawati kila shule

Na Ibrahim Joseph, DODOMA

MAMLAKA za Serikali za Mitaa nchini, zimeagizwa kuhakikisha wanafanya tathmini kwenye kila shule ili kubaini madawati ambayo yameharibika na kuyafanyia ukarabati haraka kupitia fedha za elimu bure.

Agizo hilo lilitolewa juzi na Waziri wa Nchi , Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, alipokuwa akipokea taarifa ya utafiti uliofanywa na wahadhiri wa Chuo Kikuu cha Dodoma (Udom) kuhusu sekta ya elimu mkoani Dodoma.

Jafo aliwataka wakurungenzi wa halmashauri kupita kwenye shule zao zote zilizopo kwenye maeneo yao kubaini madawati na thamani za shule zilizoharibika zinafanyiwa ukarabati.

"Hatuwezi tukasubiri madawati mapya yaje, sawa tutaendelea kununua madawati mapya, lakini wakati yale yaliyoharibika yanaendelea kufanyiwa ukarabati ili yaendelee kutumika,"alisema.

Alisema kutokana na utafiti uliofanywa na wahadhiri hao, umebaini kuwa kuna madawati mengi , viti na meza pamoja na baadhi ya samani za ofisi zimeendelea kukaa kwenye vyumba wakati vinahitaji ukarabati mdogo jambo ambalo lipo ndani ya uwezo wa fedha zinazotolewa na serikali za elimu bure. Alibainisha kuwa kuna baadhi ya samani hizo za ofisi zinahitaji ukarabati mdogo hivyo kupitia fedha za elimu bure zinazotolewa na serikali kamati za shule zitapitia na kutenga fedha za ukarabati wa vifaa hivyo.

Hata hivyo, alisema ukarabati huo unatakiwa kwenda sambamba na ukarabati wa miundombinu ya shule zote ambazo majengo yake yamechakaa kutokana na kuwa ni ya muda mrefu.

"Leo hii shule zetu zingine darasa tangu limejengwa mwaka 1980 mpaka leo hii darasa halijakarabatiwa, darasa la wahenga halitii hata hamu walimu kufundisha, watu wanaona darasa linachaka tofali linadondoka lakini hawataki kufanya ukarabati hatuwezi kuendelea kuvumilia hali hii kuendelea,"alisema.

Waziri Jafo alisisitiza kuwa kuna baadhi ya vyumba vilivyojengwa vizuri ya majengo ya shule vimekuwa vikiharibika kutokana na kutofanyiwa ukarabati haraka na kuchangia kuharibika kwa jengo zima.

Awali, akiwasilisha utafiti huo, Mhadhiri na kiongozi wa utafiti kutoka Udom, Dk. Ombeni Msuya alisema utafiti huo umefanyika kwenye shule za sekondari za Mkoa wa Dodoma kuangalia samani za shule ikiwemo meza, viti, kompyuta majengo na miundombinu mingine.

Dk. Msuya alisema katika utafiti huo walipita baadhi ya shule katika mkoa wa huo na kubaini kuwa kuna kati ya viti 11,939 vilivyopo ni 927 vibovu, meza zilizopo 10,868 kati ya hizo 690 ni mbovu huku kati ya kompyuta 100 zilizopo 16 ni mbovu.

Alishauri kamati za shule , walimu na wananchi kushirikiana katika kulinda mali na vifaa vya shule pamoja na kufanya matengenezo vifaa hivyo ili kupunguza upungufu uliopo.

Kwa upande wake, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge aliwapongeza wahadhiri hao kwa kufanya utafiti huo utakaosaidia kuboresha sekta ya elimu huku akiwaomba wahadhiri wa vyuo vikuu vingine nchini kuiga mfano huo.

## UWT yahimiza Dodoma kijani

Na Mwandishi wetu, DODOMA

UMOJA wa wanawake wa Chama cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Dodoma, umewataka wananchi kupanda miti kwenye maeneo yao ili kuufanya mkoa huo kuwa wa kijani na kupunguza hatari ya ongezeko la joto nchini.

Wito huo ulitolewa na Mwenyekiti wa UWT Mkoa, Neema Majule, alipokuwa akizungumzia kampeni ya upandaji miti miche 15,000 katika wilaya saba za mkoa huo.

Alisema upandaji miti itasaidia kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi huku akiwataka wanawake kuwa mabalozi muhimu wa kurejesha rutuba ya ardhi kwa kupanda miti katika makazi yao.

Mwenyekiti huyo, alisema Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, alishaonyesha njia ya kuikijanisha Dodoma hivyo ni wajibu wao kubeba dhamira yake kwa vitendo.

"Tupande miti ya matunda na kivuli katika shule zetu, hospitali, kwenye makazi yetu na maeneo mengine,"alisisitiza.

Majule alihimiza kuitunza miti hiyo ili ni kuleta matokeo yaliyokusudiwa.

Mbali na hilo, Mwenyekiti huyo aliwataka wanawake kusimamia suala la malezi ya watoto wao ili wafikie ndoto zao kimasomo.

Awali, Katibu wa UWT Mkoa huo, Sophia Kiwanga, alisema upandaji miti hiyo umefanyika katika wilaya ya Dodoma mjini, Kondoa, Chemba, Mpwapwa, Chamwino, Kongwa na Bahi.

Alisema pamoja na kupanda miti walitumia fursa hiyo kuzungumza na akina mama, wanafunzi hasa wasichana ili wajitambue na kuona thamani waliyonayo mbele ya jamii.



Ofisa Masoko wa Jiji la Dodoma, James Yuna akitoa taarifa kwa waandishi wa habari jijini humo juzi, kuhusu zoezi linaloendelea la kuviondoa vibanda vya wafanyabiashara ndogondogo maarufu kama machinga, waliojenga kinyume na sheria za jiji. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Mkuu wa Magereza akomalia kila gereza nchini kujitegemea

Na Renatha Msungu, DODOMA

MKUU wa Jeshi la Magereza nchini, Kamishna Jenerali Suleiman Mzee, ameagiza kila gereza kubuni kitega uchumi ili kujiendesha kwa kutumia rasilimali zake na si kutegemea serikali.

Kamishna Jenerali Mzee alitoa agizo hilo jana alipotembelea miradi inayotekelezwa na Magereza Mkoa wa Dodoma ikiwamo mradi wa ufyatuaji tofali na ujenzi wa nyumba 20 za maafisa wa magereza.

Akikagua miradi hiyo, Mkuu huyo alipongeza jitihada zinazofanywa na mkoa huo huku akitaka na mikoa mingine kuiga utendaji huo ili kila gereza lijitegemee kwa kila kitu bila kutegemea serikali kujiendesha.

Alisema Magereza ina rasilimali na nguvu kazi ya kutosha kwa kubuni miradi kulingana na jiografia kwenye maeneo yao.

" Tulikuwa na kikao na wakuu wa Magereza nchi nzima hapa Dodoma na katika kikao hicho nimesisitiza kuhakikisha kila gereza linajitegemea na kuwa na miradi ya kujiendesha,"alisisitiza.

Aliongeza "Sio kila mkoa lazima mlime au mfuge kila mkoa una jiografia yake kila mkoa uone katika mkoa wake wataanzisha nini kitakachopelekea kujitegemea."

Mkuu huyo alisema jeshi hilo lina miradi mingi kupitia Shirika lake la Magereza ambapo kuna vitega uchumi vingi ikiwemo mashamba, mifugo ya aina mbalimbali na kila mkoa una wajibu wa kusimamia.

Kwa upande wake, Mkuu wa Magereza Mkoa wa Dodoma, Keneth Mwambije, alisema ujenzi wa nyumba hizo umetumia fedha kidogo ambapo hadi kupaua zimegharimu Sh. Milioni saba.

Alisema mafanikio hayo yametokana na matumizi ya rasilimali zilizopo ikiwamo wafungwa.

"Jeshi hili limejipanga kufanya kazi zetu kwa kujitegemea bila kuomba msaada sehemu yoyote,"alisisitiza.



Mwakilishi wa Jimbo la Uzini, Muhammed Raza (kulia), akizungumza na Mwakilishi wa jimbo la Chaani, Nadil Abdullatif, nje ya ukumbi wa Baraza la Wawakilishi Chukwani Zanzibar juzi. Katikati ni Mwakilishi wa kuteuliwa na Rais, Ahmada Yahya Abdulwakil.
**PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Aibana serikali sheria zote ziandikwe kwa Kiswahili

**Na Rahma Suleiman**
ZANZIBAR

WATENDAJI wa wizara na taasisi za serikali wametakiwa kutayarisha sheria kwa Kiswahili ili wananchi wazifahamu.

Rai hiyo ilitolewa jana na Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria na Kanuni ya Baraza la Wawakilishi, Rashid Makame Shamsi, wakati akiwasilisha maoni ya kamati mbele ya wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Alisema miswada na sheria 32 imepelekwa katika kamati, lakini iliyoandikwa kwa lugha ya Kiswahili ni mitano tu, jambo ambalo ni kinyume cha kanuni na sheria za baraza hilo.

Alieleza miswada hiyo kabla ya kupelekwa Baraza la Wawakilishi inatakiwa kupelekwa kwa wananchi kwa ajili ya kuisoma na kutoa maoni. Alisema miswada kupelekwa mbele ya baraza ikiwa imeandikwa kwa lugha ya Kiingereza ni kwenda kinyume cha katiba na kanuni namba 25 ya baraza. "Mheshimiwa Spika, miswada mingi ya sheria na kanuni za baraza inaandikwa kwa lugha ya Kiingereza ambayo siyo rasmi kwa matumizi ya Baraza la Wawakilishi," alikumbusha.

Alizitaka wizara kabla ya kupeleka mswada na kusomwa mbele ya Baraza la Wawakilishi, kuhakikisha wananchi wameshirikishwa.

Alisema utafiti umefanywa na kubaini sheria nyingi zinazopitishwa mbele ya Baraza la Wawakilishi, wananchi hawazijui wakati wao ndiyo walengwa wakubwa.

"Sheria zote kabla ya kuletwa mbele ya Baraza la Wawakilishi kwanza tuwashirikishe wadau kwa kutoa maoni yao... sheria hizo walengwa na watekelezaji wakubwa ni wananchi," alisema.

# Serikali yapata dawa uboreshaji wa kilimo

**Na Rahma Suleiman**,
ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema itaendelea kujenga barabara za ndani zikiwamo zinazokwenda vijijini, ili zisaidie na kuharakisha maendeleo ya sekta ya kilimo.

Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum, Shamata Shaame Khamis, aliyasema hayo wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Chake Chake, Suleiman Said Sarahani, aliyetaka kujua lini barabara za ndani katika jimbo hilo zitafanyiwa matengenezo.

Khamis alisema barabara za ndani ni muhimu na zinafahamika na serikali kwa kuwa zinatumiwa vizuri na wananchi kwa ajili ya kurahisisha huduma za usafiri kwenda mashambani.

Alisema barabara za ndani zinashughulikiwa kwa karibu sana na serikali za halmashauri za mitaa kwa kushirikiana na idara ya ujenzi na ukaguzi wa barabara.

Alisema barabara za ndani katika Jimbo la Chake Chake ni muhimu kwa kuwa ni kiungo kikubwa kwa wananchi katika shughuli za usafirishaji.

"Nia ya serikali ni kuzifanyia matengenezo barabara zote za ndani zinazokwenda moja kwa moja kwa wananchi ili kurahisisha huduma za usafiri na kilimo," alisema.

Alisema serikali inakusudia kuzifanyia matengenezo barabara za ndani za Mkoa wa Kusini Pemba zikiwamo zile zinazokwenda moja kwa moja katika mashamba ya karafuu.

Alilipongeza Shirika la Taifa la Biashara (ZSTC) kwa kufanya ukarabati wa barabara za ndani katika mashamba ya karafuu na hivyo kusaidia uvunaji wa zao hilo.

"Tunalipongeza shirika kwa kusaidia kufanya matengenezo ya barabara za ndani zinazokwenda katika mashamba ya karafuu na hivyo kusaidia kazi za uchumaji na kufikisha zao hilo katika vituo vya ununuzi," alisema.

# Zanzibar kuruhusu kichina kutumika kufundishia

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Elimu na Mafunzo ya Amali, imesema iko katika matayarisho ya kuanza kusomeshwa kwa lugha ya kichina katika ngazi ya elimu ya sekondari kutokana na umuhimu lugha hiyo duniani.

Hayo yalisemwa na Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Simai Mohamed Said, wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Paje, Jaku Hashim Ayoub, aliyetaka kujua lini lugha hiyo itafundishwa katika ngazi ya sekondari Unguja na Pemba.

Alisema lugha ya kichina ni muhimu kutokana na mahitaji yake kwa wanafunzi katika kupata elimu ya vyuo vikuu vya China.

Alisema Wizara ya Elimu kwa sasa iko katika maandalizi ya kusomesha kwa lugha hiyo katika shule za sekondari Unguja na Pemba.


"Mheshimiwa Spika, napenda kuwajulisha wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba tunakusudia kufundisha lugha ya kichina kwa ngazi ya sekondari ili kuwaweka vizuri wanafunzi wetu watakaobahatika kwenda kusoma China kufahamu vizuri masomo yao," alisema.

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Riziki Pembe Juma, alisema tayari lugha ya kichina inafundisha vizuri katika Chuo Kikuu cha Taifa (SUZA) katika ngazi ya stashahada.

"Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kupitia Chuo Kikuu cha (SUZA) tayari tunafundisha lugha ya kichina kwa wanafunzi wa elimu ya stashahada ya lugha," alisema.

Alisema hivi karibuni alifanya ziara katika vyuo vikuu vya China na kujenga ushirikiano ambao suala la kuimarishwa kwa lugha ya kichina na kufundishwa katika shule za sekondari lilizungumzwa.

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE
JUMAMOSI FEBRUARI 22, 2020



**HONGERA OLAMIDE KUPATA DILI SAFI** Soma UK.20



## SIRI YAFICHUKA

# Irene Uwoya kakataa talaka, ndoa ilijaa utata na maumivu

## BASI SAWA

# Amber Rutty chozi lako liwe la kweli

MSANII na Video Vixen hapa nchini, Amber Rutty, amemwaga chozi na kusema kuna baadhi ya watu wanatamani asiwepo duniani kwa kumchukia.

Amber Rutty amejitoa mhanga kwa kuwaomba msamaha Watanzania na kutaka watu wampokee na kukubalika katika jamii.

"Mimi nimekuwa mtu wa kupata matatizo kila siku kwenye maisha yangu yote, kuanzia ututoni hadi hapa nilipofikia, ninachoweza kusema kwa ndugu, jamaa, na Watanzania wote wanisamehe maana sijaona kosa langu lilipo, japo watu wananichukia na kuniona binadamu mkosefu kuliko mtu yeyote hapa duniani" ameeleza Amber Rutty.




# Mh! Snura kweli una Alkasusu?

MSANII wa filamu na muziki, Snura Mushi, amesema vitu vya kuongeza nguvu za kiume kama Alkasusu, tende na mihogo mibichi vinapatikana kwake.

Snura amesema hayo kupitia show ya Planet Bongo ya East Africa Radio, kwamba vitu hivyo hadimu huwa anampa mpenzi wake Minu Calypto, na si mtu mwingine.

"Mambo hayo ya Alkasusu, Urojo, juisi ya tende na mihogo mibichi vyote vipo mwilini akinigusa tu anavipata, kila siku kwetu ni Valentine Day penzi letu lipo juu kama dirisha, halafu kuhusu umri nimemzidi miaka kidogo sio mingi kihivyo kama watu wanavyofikiria" amesema Snura Mushi.





# Vanessa hajitambui kwa Rotimi

MREMBO anayeendelea kufanya vyema ndani na nje ya nchi, Vanessa Mdee, maarufu kwa jina la Vee Money' amesema ndoto yake imetimia baada ya kumpata mwanamume mwenye hofu ya Mungu.

Mdee kwa sasa yupo katika penzi zito na Olurotimi Akinosho 'Rotimi' ambaye ni mwingizaji na mwimbaji Marekani mwenye asili ya Nigeria.

Staa huyo amesema alitumia muda mrefi kumuomba Mungu juu ya kupata mwanamume aliyekuwa sahihi kwake, huku akizingatia zaidi mtu ambaye atakuwa na hofu ya Mungu.

"Sasa ile ndoto yangu imetimia kupata mwanamume mwenye hofu ya Mungu na mwenye busara, Rotimi najifunza mengi kutoka kwake na kufurahia mapenzi yetu," alisema.

## INSTA-TWITTER





Ikiwa kuna kosa unahisi nimetenda niite uniseme kuliko kukaa pembeni kunisema vibaya-**Isha Mashauzi.**



Ni mashauzi tu kwa kuwa nilikuwa kwenye maeneo ya dola. Ila sikulipa mimi yakhe. Mtoto kalipiwa huyo-**Jackline Wolper.**

## UNASEMAAA...

### JITU BAYA

# Mbadala wa Chidi Benz anayekuja kwa kasi



ANAITWA Isahaka Hamad, lakini kwa jina la kisanii anafahamika kama 'Jitu baya', kutokana na kipaji chake katika muziki wa Hip hop anafananishwa na mkongwe Chid Benz.

Jitu baya ambaye ametoa singo yake 'Flow Kali', unapomsikiliza kwa haraka jinsi anapofokafoka unaweza kudhani sauti unayoisikia ni yule mkali Chidi Benz ambaye kwa sasa anahangaika kuachana na matumizi ya dawa ya kulevya.

Akizungumza na BT, Jitu Baya anasema watu wengi waliosikiliza nyimbo yake wanaamini ameimba Chid. lakini ukweli ni sauti yake halisi ila imefanana na msanii huyo.

"Watu wanafananisha sauti yangu na Chidi Benz, nafurahi kuwa na sauti ya aina hiyo kwani inanifanya nijione fahari kufanana na mwanamuziki mkubwa na aliyewahi kutamba katika muziki wa hip hop hapa nchini," amesema Jitu Baya.

Amesema singo yake inayoitwa 'Flow Kali' ni utambulisho wake kwa mashabiki wa muziki wa kizazi kipya wakati anajiandaa kutambulisha kazi zingine hivi karibuni.

Jitu Baya alianza kupambana katika muziki mwaka 2000, ilipofika 2018 alikamilisha wimbo wake wa kwanza uliorekodiwa na Masa studio chini ya mtayarishaji E Music.

**SITAKI BIFU**

Msanii huyo amesema katika vitu ambavyo anavichukia ni kutengeneza na kuwekeana mabifu kwa wasanii wa Bongo fleva.

Amesema mara nyingi mabifu yanajenga chuki na kuondoa ushirikiano ambao unaweza kuwanyanyua wasanii wakubwa na wale chipukizi.

"katika vitu ninavyochukia ni kuwekeana bifu kwa wasanii, upande wangu naona hakuna tija badala yake inazidisha uhasama," amesema.



# Nini ungesema hayo mwanzoni yasingekukuta

MSANII wa kike wa Bongo fleva, Nini amesema hajawahi kutoa ujauzito wa Nay wa Mitego na sasa hivi yupo tayari kubeba ujauzito wa mwanamume yeyote.

Akizungumza na EATV, Nini amesema amekuwa akituhumiwa kutoa ujauzito wa Nay wa Mitego, tangu mwaka 2017, jambo ambalo sio la ukweli kwani hata yeye anatamani kuwa na mtoto.

"Kwanini nitoe mimba, sina sababu ya kufanya hivyo, mimi bado mdogo halafu Nay ni baba mzuri kwa watoto wake, namuona jinsi anavyowalea, hata nikisema niwe na mtoto najua atakuwa kwenye mikono salama, kuna watu kila siku wanataka watoto hawapati" amesema Nini.



# Ben Pol hata ungekwenda usingesema

STAA wa muziki wa kizazi kipya, Benard Paul, maarufu kama `Ben-pol` amesema kufanikiwa au kutofanikiwa katika tasnia hiyo ni mapenzi ya mungu.

BenPol ambaye anatamba na wimbo wake mpya 'Ebenezer' amesema amewahi kuwa na marafiki ambao walimshawishi kwenda kwa waganga ili atoke kimuziki, lakini kutokana na imani yake alikataa.

"Katika maisha kuna changamoto nyingi, ukizingatia marafiki kuna wenye nia nzuri na mbaya, nimewahi kukutana na wenye nia mbaya walitaka kunipeleka kwa waganga ili niweze kutoka kimuziki," alisema.

## INSTA-TWITTER



**Tumsifu** bwana kwanza, kuwa mpekwe, kukataliwa, kuachwa, kuacha yote ni matokeo ya dunia tu-**Diana Kimaro.**



**Bwana** wetu aliye hai huangalia kila bawa lake na kuhakikisha liko sawa, wewe ni moja kati ya mbawa hizo hivyo usilalamike..Usihuzunike wala kukata tamaa na maana yeye ashinda yeyote yuko pamoja nawe muda wote-**Aunt Ezekiel.**



**Usiseme** mwaka huu tutakufa njaa. Sema mwaka huu nitakufa njaa. Wakati unalalamika njaa, wenzio wana 'stock' kubwa ya mahindi, maharage na mifugo kwa ajili ya nyama choma za hapa na pale, hivyo pambana-**Linex Mjeda.**

Kuumbe!



SIRI YAFICHUKA

# Irene Uwoya kakataa talaka, ndoa ilijaa utata na maumivu

SIRI iliyojificha kuhusu ndoa ya mastaa, Dogo Janja na Irene Uwoya, sasa imefichuka baada ya kujulikana kwamba harusi yao haikuwa halali.

Dogo Janja ambaye ni mwanamuziki wa Bongofleva na Uwoya anayetamba katika uigizaji, walifunga ndoa na kuachana katika kipindi cha mwaka mmoja.

Akizungumza na Ayo Tv, Uwoya, amesema kutokana na utata wa ndoa yao, haihitaji kupewa talaka kama wanavyofanya wanandoa wengine.

"Kutokana na mazingira ya ndoa yenyewe sidhani kama nahitaji kupokea talaka, ipo vigumu sana," amesema Uwoya ambaye hivi karibuni ametambulisha filamu yake mpya inayoitwa I Dance.

Amefichua kwamba hata yeye haamini kama ndoa yao ilikuwa sawa hasa kutokana imani zao kuwa tofauti.

"Sijawahi kubadili dini na ndio maana nasema sihitaji kupewa kitu kama hicho, kila mtu aliamua kuondoka na mimi ndiye wa kwanza kuhama nyumba," ameongeza.

Bila kumtaja jina, Uwoya anasema huwa hampendi mwanaume muongo au muongeaji sana katika maisha yake.

"Sipendi mwanamume muongo na muongeaji sana, kuna wanaume wengine wanaongea hata siku mnatoka na rafiki zako, yeye huwa anadakia maongezi hata kama hayamuhusu," akaeleza.

Akizungumzia hatma yake ya mapenzi, amesema yupo tayari kuolewa ndoa ya tatu kwani anaona jambo hilo ni Baraka.

Hata hivyo, ametoa onyo kwamba yeye hapendi mume atakayemuumiza kwa kutoka nje kimapenzi, kwani huwa anaumia sana.

"Ninapoumizwa huwa napaniki sana, nikimpenda mtu napenda sana, huwa naumia sana. Baada ya hapo nikiamua kubadilika nakuwa na roho ngumu, nachukia sana," amezidi kusema.





# Zilipendwa zinazowachengua vijana

**Na Adam Fungamwango**

NI ukweli usiopingika kuwa nyimbo nyingi za zamani zimekuwa na maudhui yasiyochuja au kupitwa na wakati.

Wanamuziki wa zamani walizungumzia mapenzi, afya, elimu, uhusiano ya kijamii, majanga, misiba, siasa na mengi yanayofanana na hayo. Ndiyo maana hadi leo zinapotokea shughuli za kisiasa kama Muungano, Uhuru na nyingine, nyimbo zinazotamba ni za muziki wa zamani na dansi.

Hata unapotokea msiba wa kitaifa, nyimbo zinazochukua nafasi za maombolezo zinakuwa ni za zamani kwa sababu wao waliangazia sehemu nyingi.

Utashangaa, lakini ni ukweli usiopingika kuwa, baadhi ya nyimbo za zamani zimepata bahati ya kupendwa mno na kurithiwa kizazi hadi kizazi, kiasi kwamba hata ikipigwa leo, pamoja na kwamba ulirekodiwa miaka 30 au zaidi iliyopita, lakini kijana wa miaka 18 hadi 25 anaweza kukuimbia mwanzo hadi mwisho, tena kwa hisia na pia kuonyesha kabisa kuwa anauhusudu.

Hizi ni baadhi ya nyimbo tano ambazo zilipigwa zamani, lakini zinapendwa hata na vijana wa kizazi cha sasa.

**RANGI YA CHUNGWA-NYANYEMBE JAZZ**

Ni wimbo uliorekodiwa mwaka 1975 na bendi ndogo tu ya Nyanyembe Jazz ya mjini Tabora.

Hata hao watu wazima si wengi wanaoifahamu bendi hiyo, lakini wimbo huo umeendelea kuwa maarufu zaidi kwa miaka 45 sasa.

Ni wimbo ambao ukipigwa kwenye redio, hata watoto wanaonekana kupenda na kuukubali. Kwenye bendi mbalimbali nchini, kama wimbo huu haikupigwa basi hilo dansi halijaisha bado.

Mtunzi wa wimbo huu, Mzee Kitambi kwa sasa yupo Dar es Salaam, akisaka hatimiliki ya wimbo wake ili awe analipwa, kutokana na wimbo huo wa 'Rangi ya Chungwa' kutumiwa sana na bendi nyingi ambazo zimeurekodi tena.

**GEORGINA-SAFARI TRIPPERS**

Huu nao ni mmoja wa wimbo maarufu sana mithili ya wimbo wa taifa. Hakuna kijana wa sasa ambaye haujui wimbo huu. Hautofautiani sana na 'Rangi ya Chungwa'. Nao unapigwa sasa kwenye bendi mbalimbali zinazopiga muziki wa laivu.

'Georgina' unashindana na wimbo huo kuombwa na mashabiki na wengi ni vijana wa kizazi cha sasa, licha ya kwamba nao ulirekodiwa mwaka 1976 na bendi ya Safari Trippers, ukitungwa na Jumanne Uvuruge na kuimbwa na hayati Marijani Rajab.

**KARUBANDIKA-MAQUIZ ORIGINAL**

Si tu kwamba wimbo huu ni maarufu zaidi Tanzania, lakini hata nchini Kenya. Mtunzi mwenyewe Kasaloo Kyanga kabla umauti haujamkumba, alisema kuwa alikwenda nchini Kenya na kuukuta wimbo huo unapigwa kwenye kila bendi ya laivu. Lakini alipowaambia kuwa yeye ndiye mtunzi wa wimbo huo, walionyesha shaka, lakini alipokuwa akipanda jukwaani na kuuimba, ndipo wanapokubali kwa sababu ya sauti yake ndiyo ile halisia wanayoisikia kwenye redio.

Hapa Bongo, vijana wengi wa kizazi cha sasa wanaufahamu sana wimbo huu na kuuimba mitaani, japo ulitungwa mwanzoni mwa miaka ya '90.

**SINA MAKOSA-LES WANYIKA.**

Wimbo wa 'Sina Makosa' nao ni moja ya ngoma ambazo vijana wa kisasa hawapati hata tabu kuufahamu.

Ni wimbo maarufu sana mitaani hata kwa watoto wadogo. Kwenye bendi za laivu huu ni kipenzi zaidi kwa wasichana miaka 18 hadi 25 ambazo wamekuwa wakiuomba, kuucheza na kuuimba, unaweza ukadhani kwamba umetungwa kipindi hiki hiki cha kina Ali Kiba na Harmonize, wakati ulitungwa mwishoni mwa miaka ya '70.

Les Wanyika ni bendi ya Kenya, lakini bendi ya Watanzania na wanamuziki wake wote ni Wabongo wakiongozwa na kina Profesa Omari, John Ngereza na wengineo.

**MTAA WA SABA-MBARAKA MWINSHEHE**

Wimbo huu uliotungwa miaka ya '70, ulipata umaarufu sana kwenye miaka ya 2000, baada ya kituo cha tevevisheni cha East Afrika kuupiga, huku wachekeshaji wakiucheza.

Hii ilisababisha vijana na watoto wengi kuujua na kuanza kuuimba mitaani na hata kuigiza jinsi ya uchezaji wa wale jamaa, hivyo kuufanya uwe unapigwa hadi kwenye sherehe mbalimbali za kijamii.

Nao ni moja ya nyimbo maarufu sana za zamani zinazotambuliwa na vijana wa kizazi cha sasa.

IMETOKEA

# Unene wawaponza, wakataliwa kukalia viti vya daraja la kwanza

KUKALIA viti vya daraja la kwanza kwenye ndege inayosafiri kwa umbali wa saa 11 ni jambo la kufurahia.

Hata kwa Renell na Tere waliokuwa wakirudi Aucland, walitarajia jambo hilo wakati walipokuwa wakitoka Bangkok kurudi nchini kwao baada ya kufanyiwa upasuaji wa kupunguza unene.

Badala yake dada hao wawili pamoja na mama yao, Huhana walikuwa na kiwewe baada ya wafanyakazi wa kampuni ya ndege ya Thai walipokwenda mbele yao na mkanda wa kipimo na kuwaambia ni wanene kupita kiasi, hivyo hawawezi kukaa katika viti hivyo vya kifahari.

Lakini miezi sita baada ya tukio hilo, Huhana mwenye umri wa miaka 59 amekuwa na uchungu kuhusu kitendo hicho na kuamua kuweka wazi .

"Wafanyakazi walipiga kelele mara kwa mara wakisema tumenenepa sana. Watu walitutazama tukipimwa katika eneo la kuingia ndani ya uwanja wa ndege". amesema

"Ilikuwa aibu kubwa jinsi tulivyofanyiwa hatua ilionifanya kudondokwa na machozi", ameongeza Huhana.

Tatizo la kutojua lugha waliokuwa wakitumia liliwafanya wasifahamu kila neno walilotamka, lakini wafanyakazi walikataa kuwaruhusu kukalia viti hivyo na kuwalazimu kuketi katika viti vya kawaida.

Huhana anasema kwamba hatosafiri tena kwa ndege, hadi pale atakapopunguza uzani, ili kuzuia uchungu alioupata yeye na watoto wake.

Kampuni nyingi za ndege huongeza urefu wa mikanda ya viti kwa abiria walio na uzito mkubwa.

Lakini kampuni ya ndege ya Thai ilisema kwamba mikanda katika viti vyake vya kifahari haiwezi kuongezwa urefu. Familia hiyo bado imeshangazwa na maelezo hayo. IMAGES

Tangu kisa hicho Huhana na wanawe wamekuwa wakijaribu kudai kulipwa fedha kutoka kwa kampuni ya ndege ya Thai kwa kuwadhalilisha.

Lakini kampuni hiyo imesema kwamba itawalipa salio la bei ya viti vya daraja la kwanza na vile vya daraja la pili.

Shirika hilo lilimfuata wakala aliyeuza tiketi hizo na kumlipa salio ya pesa, hata hivyo familia hiyo ililazimika kusubiri kwa takriban miezi sita kuzipata.

Walipowasiliana na BBC, msemaji wa kampuni ya ndege ya Thai, alisema kwamba kwa sasa wana mifumo mizuri ya tahadhari na hata mawakala huelezewa.

Familia hiyo ilikuwa katika ziara ilioandaliwa na Destinationa beauty, ambayo husimamia kuwapeleka wateja Thailand ili kufanyiwa upasuaji wa kupunguza uzani.

Martin Olsen, Ofisa Mkuu wa kampuni ya Destination Beauty , alisema kwamba alihuzunishwa sana jinsi kampuni hiyo ilivyolichukulia swala lote.

Pia alishangazwa na vitendo vya wafanyakazi wa Thai Airways , kwa kuwa watu wengi walionenepa kupitia kiasi hukalia viti vya daraja la kwanza badala ya viti vya kawaida.





Deception

# Usiendekeze moyo

**Na Adam Fungamwango**

LEO ngoja turudi nyuma kidogo, enzi za uhai wa nguli wa sanaa za filamu, hayati Steven Kanumba kwenye moja kati ya kazi zake bora kabisa.

Filamu hii inaitwa 'Deception'.

Wakati mwingine binadamu unaweza kupata matatizo makubwa. Watu unaowaamini wanaweza kukufanyia mambo ambayo hukutarajia .

Mara nyingi hapo mtu hujawa na hasira na kuweza kufanya jambo lolote lile baya, ili mradi tu kuonyesha kuchukizwa na kile ulichofanyiwa.

Hata hivyo tunashauriwa kuwa chochote ambacho binadamu anafanyiwa kibaya, anapaswa ama kumshitakiwa Mwenyezi Mungu, au kupeleka suala lake kwenye vyombo vya sheria, au kufanya vyote viwili, lakini si kujichukulia sheria mikononi, moyo unavyokutuma.

Hili limeonekana kwenye filamu ya 'Deception'. Imechezwa na Kanumba mwenyewe, aliyekuwa rafiki yake mkubwa Patcho Mwamba, Rose Ndauka, Sethi Bosco na wengineo.

Patcho na mkewe Rose wanaishi maisha mazuri, wakiwa na kila kitu ambacho kinahitajiwa ili ndoa yao iwe na furaha na amani. Wana nyumba nzuri, gari pamoja na maisha ya kifahari.

Hata hivyo mwanamama huyo anaingia kwenye penzi na jamaa mmoja wa mtaani ambaye hata pesa zake za kutanua tu, anazipata kwa kumuomba mama yake.

Huyu si mwingine bali na Kanumba. Anaiingilia ndoa ya Patcho, kiasi mpaka mwenyewe anahisi kuwa kuna kitu ambacho si cha kawaida.

Kuna siku Rose anapigiwa simu kutoka Songea kuwa mama yake ni mgonjwa sana kiasi kwamba anatakiwa aende haraka sana kumuuguza.

Haikuwa hivyo, Simu ile ilikuwa ni magumashi matupu. Ilitengenezwa tu ili aende kutanua na mpenzi wake Kanumba.

Pamoja na Patcho kumsindikiza mkewe hadi kwenye kituo cha mabasi Ubungo na kuhakikisha mpaka basi linaondoka, Rose anashukia njiani na kwenda moja kwa moja hadi kwa mpenzi wake Kanumba. Wanakwenda kwenye hoteli moja maarufu hapa jijini kwenda kustarehe, hadi siku alizopewa mwanamama huyo na mumewe kuuguza mgonjwa zimalizike.

Asubuhi wakati Kanumba anakwenda kuagiza supu kwa ajili ya mpenzi wake, aliporejea anamkuta amekuwa maiti. Anachanganyikiwa hajui nini kimetokea. Anatoroka, lakini anaangusha kitambulisho.

Mlinzi Seth, anamnong'oneza mmoja wa wahudumu kuwa mteja wao hakufa kifo cha kawaida, bali aliuawa na muuaji aliwahi kumuona.

Siku mbili baadaye naye anauawa akiwa hospitalini alipokuwa amelazwa. Lakini muuaji anasahau simu. Polisi wanapigiwa simu muuaji wa mgonjwa hospitalini amesahau simu, lakini wanapofika daktari anawaambia kuwa walivamiwa na mtu mmoja mwenye silaha ambaye aliwanyang'anya simu.

Mauaji hayo yanawaumiza kichwa polisi. Hata hivyo kuna mtu mmoja anajitokeza polisi na kusema kuwa ana mkanda wote wa mauaji hayo.

Anawaambia kuwa yeye mwenyewe amelishwa sumu, hivyo wakati wowote anaweza kufa, hivyo ameona kabla hajafa, ayaanike yote.

Akasema kuwa mauaji yote hayo yanafanya na kikundi kimoja ambacho kinaongozwa na Patcho Mwamba.

Akasema Patcho ndiye aliyemuua mkewe Rose pale hotelini. Filamu anaanza kuonyesha jinsi Patcho alipoingia kwenye hoteli hiyo na kumuua mkewe bila upinzani mkubwa, ingawa alionekana na Seth ambaye naye baadaye alipopata taarifa hizo alituma watu wakamuue.



WAMEANZA KUONJA CHUNGU

# Prince Harry, Meghan wapata pigo la kwanza

MWIGIZAJI wa filamu Meghan Markle na mume wake Mwanamfalme wa Uingereza, Harry, wameanza kupiga hatua kutoka katika ufalme huo baada ya taarifa kudai wamepigwa marufuku kutumia jina 'Sussex Royal' kama utambulisho wao.

Taarifa hizo zinadai kwamba Harry na mkewe, Meghan Markle, wote hawatatumia jina hilo ambalo ni sehemu ya utambulisho wao katika ukoo huo wa kifalme.

Mapema mwaka huu wanandoa hao waliishangaza dunia baada ya kutangaza nia yao ya kujitoa katika shughuli za kiflame na badala yake wanataka kuishi maisha ya kawaida.

Taarifa hiyo ambayo iliwagawanya Waingereza wengi, ilisababisha Malkia Elizabeth wa Uingereza kuitisha kikao cha ukoo wa kifalme kujadili na kisha kutoa kauli ya kukubaliana nao.

Kulingana na mtandao wa PageSix, Malkia wa Uingereza na washiriki wengine wa familia ya kifalme wamekubaliana kuwa wanandoa hao hawataweza tena kuweka neno "kifalme" kama sehemu ya chapa yao.

Katika barua moja inaripoti kuwa wenzi hao walikuwa wamepanga kuongeza jina la 'Sussex Royal' kuwa chapa yao ya kimataifa katika shughuli kadhaa, ikiwamo mavazi, vifaa vya kufundishia na vitabu.

Jina hilo pia walitaka kulitumia katika shirika lao jipya la hisani.

Chanzo kilicho karibu na familia ya kifalme kimeiambia Page Six kwamba majadiliano bado yanaendelea kwani hakuna chochote ambacho kimefanyika rasmi.

"Kama Duke na Duchess wa Sussex watarudi nyuma kuwa kama wanachama wa juu wa Familia ya kifalme na kufanya kazi wakiwa huru kifedha, matumizi ya neno 'Royal', kwa muktadha huu, yanahitajika kukaguliwa," chanzo kilisema.

Itakumbukwa kuwa mnamo Januari 2020, Prince Harry na mkewe Meghan Markle walishtua ulimwengu wakati walipongaza kwamba watajiondoa katika kazi za familia ya kifalme.

Wanandoa hao walitangaza habari hiyo ya kushangaza kupitia ukurasa wao rasmi wa Instagram na kueleza nia yao ya kwenda kuishi katika nchi mbili za Canada na Uingereza.

Prince Harry na Meghan Markle walifunga ndoa mwaka 2018 kwenye harusi iliyojaa nyota wengi.

Katika maisha yao wamefanikiwa kuwa na mtoto mmoja Archie ambaye alizaliwa mwishoni mwa mwaka jana.




# Kazi ya Burna Boy yatetewa

MREMBO anayetamba katika mitandao ya kijamii, Uti Nwachukwu, amesema ni jambo la kuvunia kuwa na mwanamuziki Burna Boy, kutokana na kuitangaza nchi yao kimataifa.

Kulingana na Uti ni kwamba Wanigeria wanatakiwa kumshukuru mwimbaji huyo kutokana na kuliweka vizuri jina la nchi yao.

Akiandika maoni yake kupitia akaunti ya Twitter kwamba mkali huyo wa Afro Beat amekuwa akitengeneza njia kwa wanamuziki wengine kwenda nje kufanya kazi za muziki.




## Brymo usemacho ni kweli?

MWIMBAJI nyota wa Nigeria, Brymo, amewashauri watu ambao wapo katika uhusiano, kipaumbele chao cha kwanza kiwe kwenye mapenzi.

Nyota huyo aliamua kutoa ushauri huo kupitia ukurasa wake wa Twitter, ambapo amesema kama mtu hutaki kushiriki mapenzi, basi ni bora kuwa karibu na ndugu zake.

"Ikiwa hutaki mapenzi nenda ukaishi na ndugu zako, huo ni upendo, kivutio cha kimapenzi ni hatua ya uhusiano utaibuka wakati mawasiliano ya mwili yatakapokuwa makali," amesema.

## Hongera Olamide kupata dili safi

RAPA kutoka Nigeria, Olamide Adedeji, amepata dili nono baada ya kutiliana saini na lebo ya kimataifa kwa ajili ya kusimamia kazi zake.

Olamide amesaini lebo ya kimataifa ya Empire, na kukaribishwa rasmi kufanya nao kazi hasa katika tasnia ya muziki wa nchi hiyo.

Muziki umekuwa katika ushindani mkubwa ndani ya nchi hiyo, ambapo kila msanii amekuwa akitafuta fursa kutoka nje ili kukuza majina yao.





## Jaywon kumbe unapenda misosi

MWANAMUZIKI wa Nigeria, Jaywon, amesema hakuna mwanamume ambaye angependa kumuoa mwanamke asiyejua kupika chakula.

Nyota huyo wa muziki ametumia ukurasa wake wa Instagram na kueleza wanaume wengi wangepeta kuajiri wapishi, lakini mwanamke anayeweza kazi za ndani ndiye chaguo zuri.

"Wanaume wangapi wanaojitokeza kujivunia na kusema mke wangu hawezi kupika au kuangalia nyumba? Ni wazi kwamba hakuna anayependa kuwa na wanawake wa aina hiyo," amesema.

## Kifo cha Patience chashtua wengi

MWIGIZAJI mkongwe wa Nollywood, Patience Oseni, amefariki dunia baada ya kuugua kwa muda mrefu.

Kulingana na mtayarishaji wa filamu, Ejiro Okurame, msanii huyo ambaye alikuwa maarufu katika tasnia hiyo alifariki siku ya Jumanne ya wiki hii majira ya asubuhi.

Kifo cha msanii huyo ambaye alisifika kwa urembo enzi zake kimeleta uzuni nchini Nigeria na nchi nyingine ambazo filamu kutoka Nollywood zinapendwa.



MAKALA



MIONZI YA SHERIA

# Ujira wa Overtime huu hapa

Na John Juma
0716217615

KATIKA saa za kazi zipo saa za kazi katika siku za kawaida, saa za kazi za ziada na saa za kazi katika siku ambazo ni za sikukuu. Kuna umuhimu mkubwa sana kwa mfanyakazi kujua saa za kazi.

Kama hujui, saa za kazi za kisheria, basi ni vigumu kujua usahihi wa ujira unaolipwa

Malipo ya kazi hayatokani na mshahara pekee. Yapo malipo mengine ya ziada yatokanayo na muda wa ziada, zikiwamo siku za sikukuu.

Ili ujue usahihi wa kile unacholipwa ya kupasa kujua pia mchanganuo wa saa za kazi. Kuna saa za kazi zao aina mbili.

Zipo saa za kazi za kawaida na saa za kazi za ziada. Sikukuu nazo hujumuishwa katika saa ya kazi za ziada.

**SAA KAWAIDA**

Katika siku za kawaida, saa za kazi ni tisa. Kwa hiyo, kwa siku mfanyakazi anatakiwa kufanya kazi kwa saa tisa. Hii ina maana, mtumishi atafanya kazi kwa saa 45 kwa wiki, ikiwa atafanya kazi kuanzia Jumatatu mpaka Ijumaa.

Cha muhimu sana katika suala la saa za kazi, kwamba mfanyakazi asifanye kazi zaidi ya saa 45 kwa wiki, katika ratiba ya saa za kawaida. Hata siku za kuwajibika, zinapozidi saa 45, inakuwa kuna makosa.

**SIKU NGAPI?**

Siku za kazi zinazoruhusiwa ni sita kwa wiki. Lakini, itategemea taratibu za ofisi. Kuna ofisi zitazomuambia anafanya kazi Jumatatu mpaka Ijumaa na wapo watakaowambia kazi ni Jumatatu mpaka Jumamosi.

Hawa wote watakuwa hawajakosea kwa sababu bado wako ndani ya ukomo wa siku za kisheria.

Linalopaswa kuzingatiwa hapo ni kuwa kwa vyovyote itakavyokuwa, saa za kazi kwa wiki zisisizidi 45. Iwe siku tano kwa wiki au sita, cha muhimu ni isizidi saa 45 kwa wiki. Hizo ni saa za kawaida. Inakuwa si saa za kawaida, bali ni ziada.

**SIKU 6-5 KAZINI**

Tumesema, saa za kazi kwa wiki zisizidi 45, iwe kwa kufanya kazi siku tano kwa wiki au sita. Hii ina maana yule anayefanya siku tano kwa wiki, atatakiwa kufanya kazi saa tisa (iwe 9 x siku 5 = 45), ambayo ni ukomo wa wiki. Lakini yule anayefanya kazi siku sita kwa wiki itatakiwa awe na saa nane kwa si kutano (yaani 8 x 5) iwe na jumla ya saa 40, labda hiyo ni Jumatatu hadi Ijumaa, halafu saa tano za Jumamosi, ili hesabu ya saa 45 kwa wiki isivuke. Hivyo, itakuwa (8 x 5= 40) halafu unajumlisha saa tano za Jumamosi, inakuiwa jumla ya saa 45 kwa wiki.

**SAA ZIADA**

Mfanyakazi anayefanya kazi saa tisa kwa siku, kwa siku sita katika wiki, anatakiwa kulipwa malipo ya saa za ziada. Atakuwa amefanya kazi jumla ya saa tisa mara siku saba (9 x siku 7 = 63) saa za jumla kwa wiki inatoka kutoka saa 45 inayotakiwa. Hivyo 63 kutoa 45(63 - 45= 18) = masaa 18 ya ziada yanayostahili malipo nje ya mshahara.

**KIASI GANI?**

Mfanyakazi atakayefanya kazi saa za ziada basi atatakiwa kulipwa 1.5 ya mshahara wake wa saa kwa kila saa lililozidi. Mshahara unaopokea, unaweza kuugawa ukaona kwa saa unalipwa kiasi gani. Ukishapata jibu chukua 1.5 ya kiasi hicho. Hiyo 1.5 ndiyo unaotakiwa kulipwa katika kila saa lililozidi.

**KAZI SIKUKUU**

Saa za kazi za siku za sikukuu ni ziada kuanzia asubuhi hadi mfanyakazi anapoondoka. Lakini, malipo ya ziada ya siku za sikukuu ni zaidi ya malipo ya ziada ya siku za kawaida.

Hapo juu tumesema 1.5 ya mshahara wa saa ndiyo hulipwa kwa kila saa lililozidi. Hata hivyo, kwa sikukuu itakuwa mara mbili yake . Itakuwa '1.5 x 2' kwa kila saa.

Yapo mengi ila haya yatoshe kwa leo. Naomba kuwasilisha!

# Utafiti waonya watoto bilioni 2.2 wataathirika

UTAFITI mpya umebaini kwamba hali ya watoto katika miaka michache inayokuja itakuwa na utata.

Kulingana na utafiti uliofanywa na Shirika la afya Duniani (WHO), unaeleza fursa ya malezi ya kiafya na mazingira yanayofaa kwa ajili ya hali zao za baadae ipo mashakani.

Wataalamu wanasema mabadiliko ya hali ya hewa na matangazo yenye dalili ya kudhuru yanayoshawishi ulaji wa vyakula vinavyopatikana kwa urahisi na unywaji wa pombe, yanawaweka watoto katika hatari.

Uingereza iliwekwa katika nafasi ya 10 miongoni mwa nchi zenye afya na hali bora ya maisha ya watoto, ilishindwa katika kuyalinda mazingira ya siku za usoni ya watoto .

Ripoti ya shirika la watoto la Umoja wa Mataifa Unicef na tume ya Lancet zilitaja nchi 180 kuwa zina uwezekano kwa watoto kukua vizuri kwa kuzingatia afya na maisha bora. Vigezo zilivyowekwa ni upatikanani wa elimu, vyakula yenye virutubisho na viwango vya vifo vya watoto.

Nchi hizo pia ziliwekwa katika viwango kwa kuzingatia uwezo wao wa utoaji wa hewa ya kaboni.

Wataalamu takriban 40 wa afya ya watoto walionya kuwa miongo miwili iliyopita itakua ya madhara ikiwa hatua madhubuti hazitachukuliwa na serikali duniani kote.

"Kila mtoto duniani kwa sasa anakabiliwa na vitisho vilivyopo kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa na shinikizo za kibiashara,"anasema Waziri Mkuu wa zamani wa New Zealand, Helen Clark, ambaye pia ni msaidizi mkuu mwenza wa tume ya Unicet ya masuala ya watoto.

" Nchi zinapaswa kubadili mitazamo ya afya ya watoto wadogo na waliotimiza umri wa kubalehe ili kuilinda dunia siku zijazo."

Wataalamu wanaonya juu ya kupanda kiwango cha nyuzi joto 4C katika viwango vya joto vya dunia ifikapo mwaka 2100, kwa kiwango cha makadirio ya sasa na kwamba kiwango hicho kinaweza kusababisha Athari mbaya za kiafya kwa vizazi vijavyo.

Kuongezeka kwa viwango vya maji ya bahari, mawimbi ya joto, ongezeko kubwa la utapiamlo na kuongezeka kwa maambukizi ya magonjwa kama vile malaria ni masuala muhimu ya kuyaangalia.

"Zaidi ya watu bilioni mbili wanaishi katika nchi ambako maendeleo yanakwamishwa na mizozo ya kibinadamu, na majanga asilia , matatizo yanayohusiana na mabadiliko ya hali ya hewa ," anasema waziri Awa Coll-Seck, kutoka Senegal.

Wakati onyo hilo likitolewa, imefahamika nchi maskini zaidi duniani ambazo zinazotoa kiwango kidogo zaidi cha gesi chafu, zilionekana kuwa zenye uwezekano mkubwa wa kukabiliwa na athari mbaya za mabadiliko ya hali ya hewa.

"Kuboresha viwango bora kwa ajili ya watoto sana hakufai kuharibu hali za maisha za siku zijazo kwa watoto duniani ," aliongeza Bwana Coll-Seck.

Marekani na Australia zilikua miongoni mwa nchi zinazozalisha hewa chafu zaidi duniani.

Ripoti hiyo pia imeelezea tisho linalowakabili watoto kutoka kwa masoko haramu ya biashara.

Ilibaini kuwa wanaonyeshwa matangazo 30,000 ya televisheni



kila mwaka, yakiwamo yale ya pombe, vyakula visivyo na virutubisho na vinywaji vyenye sukari nyingi.

Mwandishi mmoja wa tume hiyo, Anthony Costello, profesa wa Chuo Kikuu cha London nchini Uingereza , alionya kuwa ongezeko la matumizi ya mitandao ya kijamii miongoni mwa watoto wenye umri wa balehe inahatarisha kujiingiza katika soko la bidhaa hatari,

"Tuna taarifa chache na idadi juu ya kuongezeka zaidi kwa matangazo ya kibiashara ya mitandao ya kijamii na kiwango kinachowalenga watoto wetu ,"anasema.

Mnmo mwaka 2019 ripoti ilikadiria kuwa karibu watoto bilioni 2.2 na watu wazima duniani, walikua na uzito wa mwili wa kupita kiasi na zaidi ya watoto milioni 150 walidumaa katika ukuaji wao.

Ripoti hiyo ilitoa wito wa hatua mpya kuchukuliwa na viongozi wa dunia kurekebisha hali hiyo kwa ajili ya kuwalinda watoto.

MAKALA

# Tari na mkakati wa mafuta

## Yazindua mbegu bora za michikichi

Na Gerald Kitabu

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI), imezindua kanda za uzalishaji na usambazaji mbegu bora za michikichi nchi nzima, aina ya TENERA inayotajwa kuwa ni bora, inayotoa mafuta mara tano zaidi ya mbegu za kienyeji aina ya DURA.

Kuzalishwa na kusambazwa kwa mbegu hizo, katika kanda zote nchini, inalenga nchi kujitosheleza kwa mafuta ya kula na kwamba ni moja ya mikakati kabambe ya TARI kuinua uchumi wa viwanda.

Inakadiriwa kuwa mahitaji ya mafuta ya kula nchini ni tani 570,000 kwa mwaka. Kati ya tani hizo takribani asilimia 60 ya mafuta yanaagizwa kutoka nje ya nchi.

Hii ina maana kwamba ni asilimia 40 tu ndo inayozalishwa hapa nchini, na kwa mujibu wa watafiti, asilimia 60 ya mafuta ya kula kutoka nje ya nchi yanagharimu jumla ya Sh. billioni 443 kwa mwaka.

Inaelezwa kuwa hicho ni kiwango kikubwa cha fedha, ambacho TARI imeamua kuokoa kupitia mpango wake wa kuanzisha vituo vya uzalishaji katika kanda zote na kusambaza ili taifa lijitosheleze kwa mafuta ya kula.

Hii pia ina maana kwamba wakulima, ambao wanatumia mbegu za kienyeji aina ya DURA wataondokana na mbegu hizo ili waweze kuzalisha kwa tija.



Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Gelasius Byakanwa, akipanda mchikichi kama ishara ya uzinduzi wa kituo cha uzalishaji na usambazaji wa mbegu bora za zao hilo aina ya TENERA, kilichopo TARI Naliendele mkoani humo, kwa ajili ya wakulima wa mikoa ya kanda ya Kusini ya Lindi, Mtwara, na Ruvuma. Wengine ni wakurugenzi wa TARI kutoka kanda mbalimbali nchini. **PICHA: GERALD KITABU**

### UTEKELEZAJI

Katika kutekeleza mpango mkakati huo, TARI chini ya uongozi wa Mkurugenzi Mkuu wake Dk. Geoffrey Mkamilo, imezindua vituo vipya vya kuzalisha na kusambaza mbegu bora aina ya TENERA katika kanda zote.

Mkurugenzi huyo anataja kanda hizo kuwa ni za magharibi, kati, kusini na nyanda za juu kusini, na kwamba tayari mbegu bora zaidi ya milioni moja na laki tano zimeshasambazwa nchi nzima.

"Mbegu bora za TENERA ni za kisasa na zina uwezo mara tano zaidi ya mbegu za zamani za kienyeji aina ya DURA. Hizi zina uwezo wa kutoa tani tano hadi sita kwa hekta moja, wakati mbegu za kienyeji, ambazo zimekuwa zikitumiwa na wakulima katika maeneo mbalimbali nchini uwezo wake ni tani 1.6 kwa hekta moja," anasema Mkamilo.

Anasema, ili kufanikisha upatikanaji wa huduma ya mbegu bora, katika mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora, TARI ilizindua mpango huo mkoani Kigoma na kwamba Gereza la Kwitanga, Ilagala, JKT Bulombora ni baadhi ya vituo ambavyo tayari vimeanza kutumika kuzalisha na kusambaza mbegu hizo.

"Vilevile tayari halimashauri zote za Mkoa wa Kigoma zimeshafikiwa na mbegu bora, na baada ya uzinduzi katika Mkoa wa Kigoma, TARI ilifanya uzinduzi mwingine katika kituo cha utafiti wa kilimo Ilonga (TARI-Ilonga), wilayani Kilosa, Mkoani Morogoro," anasema.

Mkamilo anasema, kituo hicho cha Ilonga, kitafanya kazi ya kuzalisha mbegu na kusambaza kwa wakulima wa Mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro, Pwani na Zanzibar. Uzinduzi huo ulifanyika na kuhudhuriwa na Mkuu wa Wilaya ya Kilosa, Adam Mgoyi.

"Baada ya uzinduzi wa kanda hiyo ya Mashariki, TARI ilifanya mwingine katika kanda ya kusini kwa ajili ya uzalishaji na usambazaji wa mbegu bora katika mikoa ya Mtwara, Lindi, na Ruvuma," anasema. Anafafanua kuwa uzinduzi huo ulifanyika katika kituo cha utafiti wa Kilimo TARI-Naliendele kilichopo mkoani Mtwara na kuhudhuliwa na Mkuu wa Mkoa wa Mtwara Gelasius Byakanwa.

Anasema, kwa upande wa kanda ya nyanda za juu kusini, TARI ilifanya uzinduzi mwingine wilayani Kyela mkoani Mbeya na kuhudhuliwa na Mkuu wa Wilaya hiyo Claudia Kitta pamoja na mkuu wa Kituo cha Utafiti wa Kilimo Uyole kilichopo Mbeya, Dk. Tulole Bucheyeki.

Mkurugenzi huyo ansema, kituo cha Kyela kitakuwa chini ya uangalizi wa kituo cha utafiti wa Kilimo Uyole.

### MPANGO MKAKATI

Kuhusu mpango mkakati wa TARI, mkurugenzi huyo anasema, mpango huo una lengo la kuhakikisha uzalishaji mkubwa wa zao hilo la mchikichi ili taifa liweze kujitosheleza kwa mafuta ya kula badala ya kuagizia kutoka nje ya nchi.

Anasema, serikali ya awamu ya tano chini ya Rais John Magufuli imetenga jumla ya Sh. bilioni moja kuendeleza zao la mchikichi hapa nchini ili kuhakikisha uzalishaji wa mafuta ya kula unakuwa mkubwa.

"Hatua hiyo itasaidia kuepuka uagizaji wa mafuta ya kula kutoka nje ya nchi ambayo yanaligharimu taifa takribani Sh. bilioni 443 kwa mwaka," anasema.

Anasema mafuta yanayoagizwa yanatoka katika nchi za Malysia na Costa Rica wakati nchi ina ardhi ya kutosha na inayofaa kulima michikichi na uwezo na kwamba watalaam wa kutosha wapo.

"Kwa hiyo serikali imeliona hili kuwa ni bora juhudi za hali na mali zifanyike kuzalisha zao hili hapa nchini, ili kuokoa fedha nyingi, ambazo zingeweza kufanya shughuli nyingine za maendeleo," anasema.

Anasema, TARI imesambaza jumla ya mbegu bora zaidi ya milioni moja na laki tano na pia lengo ni kuhakikisha kufikia Mei wawe wamesambaza mbegu milioni tano na kisha mbegu bora milioni 20 ndani ya miaka mitano ijayo.

"Vituo vya kuzalisha na kusambaza mbegu bora katika kanda zote vimechaguliwa kutokana na uwepo wa watalaam, hali ya hewa nzuri kwa kilimo na ubora wa miundombinu iliyopo katika vituo hivyo," anasema.

### WAKUU WA WILAYA MIKOA

Mkurugenzi huyo anasema, Mkuu wa Wilaya ya Kilosa Mkoani Morogoro Adam Mgoyi anaipongeza TARI kwa jitihada za makusudi za kuhakikisha taifa linajitosheleza kwa mafuta ya kula.

Anasema, Kilosa ina ardhi ya kutosha yenye rutuba ya kuzalisha mazao yote ya biashara na chakula kwa hiyo ujio wa mbegu bora ni fursa kwa wananchi, wakulima na uchumi wa viwanda.

"Wilaya ya Kilosa ina zadi ya hekta 400,000 zinazofaa kwa kilimo cha mazao aina zote, lakini kati ya hizo tunalima hekta 160,000 tu, kwa hiyo nawakaribisha wakulima na wawekezaji kuwekeza katika kilimo cha zao hili la mchikichi ili kujipatia kipato cha kaya na kuongeza mapato ya halmahauri yetu kwa ujumla," anasema Mgoyi.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Kyela, Claudia Kitta anaishukuru TARI kwa jitihada zake, kwamba wakulima wamepata mkombozi kwa vile hutumia mbegu za kienyeji kwa muda mrefu na hivyo kuwakosesha kipato. "Wananchi wa Kyela wapo tayari kulima mchikichi kwa sababu ni zao lao la miaka mingi ila tatizo lilikuwa ni ukosefu wa mbegu bora zinazokomaa haraka, lakini kwa juhudi za, TARI, wamepata mkombozi wa kweli," anasema.

Kwa upande wake Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Gelasius Byakanwa, licha ya kuipongeza na kuishukuru TARI kwa umahiri wao wa kufanya utafiti, anawataka kufikiria namna ya kuanzisha viwanda ili wakulima waweze kunufaika zaidi na mnyororo wa thamani.

"Sisi tunaokaa karibu na nyie hapa Naliendele Mtwara tumeona utafiti wenye manufaa mengi. Lakini haitoshi kubakia kwenye utafiti tu, lazima mfikirie kuanzisha viwanda ili vitumie matokeo ya utafiti kutengeneza bidhaa, kutoa ajira na kuongeza uchumi wa nchi," anasema Byakanwa.

Anasema, anatambua kuwa TARI ina ardhi ya kutosha, utaalamu, ujuzi na uwezo wa kufanya utafiti wenye manufaa, hivyo wanatakachohitaji ni mtaji wa kuanzisha viwanda.

MAKALA

# Kongamano la elimu Mara

Na Sabato Kasika

## ■Wadau 500 kuchambua mbinu kupandisha ufaulu



Baadhi ya wanafunzi wa Bukima Sekondari iliopo Musoma Vijijini, wakiendelea na masomo darasani.

MKOA wa Mara unatarajia kufanya kongamano lenye lengo la kuongeza ufaulu katika shule za msingi na sekondari.

Kongamano hilo linakutanisha wadau wa elimu zaidi ya 500 kutoka ndani na nje ya mkoa huo.

Kulingana na Mkuu wa mkoa huo, Adam Malima, mkutano huo utafanyika kesho Februari 23, katika ukumbi wa Shule ya Sekondari ya Wasichana Songe iliopo mjini Musoma.

Baadhi ya wadau watakaoshiriki ni walimu wa shule za msingi na sekondari, viongozi wa sekta ya elimu kutoka halmashauri zote.

Wadau wengine ni wazazi, walezi na baadhi ya wanafunzi wa shule za msingi na sekondari, ambao nao watakuwa na nafasi ya kujadili kwa kina na kusaidia kupata ufumbuzi wa changamoto za elimu mkoani humo.

Mratibu wa kongamano hilo, Emmanuel Kisongo, anasema, wadau watakutana na kujadili kwa kina changamoto za elimu na kuzitafutia ufumbuzi wa kudumu.

Kisongo, ambaye alikuwa Ofisa Elimu wa Mkoa Mara, kwa sasa amehamishiwa Mkoa wa Ruvuma, anasema maandalizi yamekamilika kilichobaki kwa washiriki kuhudhuria.

"Mkuu wa Mkoa wa Mara ameamua kuitisha kongamano hilo na kualika wadau mbalimbali wa elimu, ili kujadili kwa kina changamoto zinazoikabili sekta ya elimu mkoani mwaka," anasema Kisongo.

### HALI YA UFAULU

Kisongo anasema, katika mtihani wa taifa wa darasa la saba wa mwaka jana, Mkoa wa Mara umekuwa wa 26 kitaifa, huku kidato cha nne ukiwa wa 25 kitaifa.

Mtaalam huyo wa elimu anasema, mkoa umekuwa ukiishia kushina nafasi hizo kutokana na kukabiliwa na changamoto mbalimbali.

"Niwaombe wadau wa elimu wajiandae kushiriki kongamano hili, wachangie maoni yao, kwani tunataka ushirikiano wa wananchi na serikali uendelee kuzaa matunda kwa ajili ya maendeleo ya elimu ya watoto wetu," anasema Kisongo.

Anasema, wadau watakaoshiriki, watapata uzoefu kutoka kwa wengine jinsi walivyofanikiwa kuboresha elimu kwenye maeneo yao na hatimaye watatoka na kitu walichojifunza na kukitumia, katika maeneo yao.

Anasema, Mkoa wa Mara una zaidi ya shule za sekondari 204, huku za msingi zikiwa ni 847, ambazo kwa pamoja zinatakiwa kuwekewa mikakati ili ziweze kuwa na matokeo mazuri.

"Profesa Sospeter Muhongo atakuwa mchokoza mada katika kongamano, sisi wadau wa elimu tutakuwa wasikilizaji na kupokea maoni na kuyaoanisha na sera ya elimu kuona kama hayapingani nayo," anasema.

Kisongo anasema, kuna haja ya kufanya mabadiliko makubwa kwenye elimu ili walimu wawe na moyo wa kufundisha.

Anasema kuna madai kwamba baadhi yao wamekata tamaa kutokana na kupata changamoto nyingi wanapokuwa kwenye vituo vya kazi.

Baadhi ya changamoto zinazoikumba sekta ya elimu mkoani Mara amezitaja kuwa ni uhaba wa mabweni, madawati, vyumba vya madarasa na wanafunzi kutembea umbali mrefu kufuata elimu.

"Changamoto nyingine ni wazazi kutochangia chakula shuleni na kusababisha watoto wao kushinda na njaa, huku wakidai kwamba serikali ishatangaza kutoa elimu bure, hivyo hawaoni sababu ya kuchangia chakula," anasema.

Aidha, anasema, utoro wa wanafunzi nao ni tatizo linaloendelea kuukumba mkoa huo kutokana na wanafunzi kuingia kazi za uvuvi, jando na ukeketaji.

"Unakuta wanafunzi wanakuwa watoro na kwenda kuvua samaki ziwani, wengine wakipelekwa na wazazi wao kwenye jadi na ukeketaji, sasa katika mazingira kama haya kiwango cha elimu kitashuka.

Anasema, Mara ina wanafunzi 60,000 wasiojua kusoma na kuandika, hivyo hayo yote yatajadiliwa na wadau wa elimu kwenye kongamano hilo na hatimaye kuibuka na suluhisho.




Mkuu wa Mkoa wa Mara, Adam Malima aliyeandaa kongamano hilo.

'Vilevile baadhi ya wazazi hawako kitu kimoja na walimu, wanageuka kuwa maadui wanapoambiwa makosa ya watoto wao, sasa katika mazingira ya aina hiyo, ufundishaji unakuwa wa shida," anasema.

Anasema changamoto hizo alizotaja na nyingine nyingi, zina mchango mkubwa katika kukwamisha maendeleo ya elimu mkoani Mara, hivyo kuna haja ya kuzijadili kwa kina.

Naye Ofisa Elimu mpya wa mkoa huo, Ephraem Simbeye, anasema anaamini kwamba kwa kushirikiana na wadau wote wa elimu mkoani humo, watamaliza changamoto zinazoikabili sekta hiyo.

"Mimi bado ni mgeni, ndiyo kwanza nimeripoti, lakini ninaamini kwamba tukishirikiana tunaweza kuuvusha mkoa wetu na kuuweka sehemu nzuri kwenye sekta ya elimu," anasema Simbeye.

Anasema ana taarifa kuwa mkoa umefanya vibaya katika mtihani wa taifa kwa miaka mitatu mfululizo, hivyo kongamano hilo linaweza kuja na suluhisho la kudumu la changamoto kwenye sekta hiyo muhimu.

Prof. Muhongo ambaye ni mchokoza mada wa kongamano hilo, ametoa wito kwa wadau wajiandae kutoa michango yao pamoja na kujifunza mbinu mbalimbali kutoka mikoa mingine.

"Ubora wa elimu itolewayo maana yake ni kuelimika na kufaulu mitihani, hivyo tujitayarishe huku tukidadisi na kujifunza kutoka kwingineko kwa ajili ya kuwa na elimu bora," Prof. Muhongo anasema.

# Baada Nkurunziza kupata mrithi...

## ■Upinzani wamkabidhi rungu Agathon Rwasa kumkabili

Na Mwandishi wetu

RAIS wa Burundi, Pierre Nkurunziza, mwaka huu anang'atuka na kumpisha kiongozi mwingine ambaye ataongoza nchi hiyo.

Nchi hiyo ambayo imekuwa haijatengemaa kiusalama, itafanya uchaguzi wake mkuu Mei 20 Mwaka huu baada ya Nkurunzinza kutawala kwa vipindi vitatu.

Ni zaidi ya wiki moja iliyopita, chama tawala CNDD-FDD, kilitangaza kumpitisha kada wake ambaye pia ni Meja Jenerali wa kijeshi, Evariste Ndayishimiye, kutetea kiti cha mstaafu huyo katika uchaguzi mkuu ujao, unaotarajiwa kufanyika wastani wa miezi mitatu ijayo.

Uchaguzi wa mwaka huu utashuhudia wagombea wakuu kutoka chama tawala cha CNDD-FDD na kile cha Upinzani cha National Congress for Liberty (CNL) vikichuana vikali.

Tayari chama cha upinzani cha CNL, kimefanya mkutano wake mkuu na kumteua kiongozi wake, Agathon Rwasa, kama mgombea wake katika uchaguzi huo wa urais.

Rwasa sasa atasimama katika uchaguzi huo wa Mei 20, huku akikumbuka majaribio yake mawili ya kuwania nafasi hiyo, hata hivyo hakufanikiwa.

Ikumbukwe kiongozi huyo mkuu wa upinzani alishiriki katika chaguzi za mwaka 2010 na 2015, laikini hakufanikiwa kupata kura za kutosha.

Hata hivyo, uchaguzi wote uliibua malalamiko kwamba wafuasi wake walikuwa wanakandamizwa.

Nkurunziza alishinda katika uchauzi wa mwaka 2015, uliosababisha maandamano yaliyochochea jaribio la kumpindua, kisa kikuu ni kutokubaliana na hatua yake ya kutawala muhula wa tatu.

Jeshi la Burundi lilidhibiti jaribio hilo la mapinduzi hayo na washiriki wake walikamatwa na baadhi waliangukia hukumu ya vifungo.

Rwasa ataingia katika uchaguzi akipambana na Jenerali Evariste Ndayishimiye, mshirika wa Nkurunziza ambaye alichaguliwa mwezi uliopita na chama tawala cha CNDD-FDD.

Hata hivyo, kabla ya uchaguzi Rwasa ameonesha uchaguzi huo kama hautakuwa wa huru na haki baada ya kuwepo na dalili ya mpango wa wapiga kura hewa.

"Tunakaribia uchaguzi, inashangaza kusikia kuwa kuna watu wanafikiria uchaguzi mdogo," aliwaambia wajumbe wa chama chake baada ya kutangazwa kwa uteuzi wake.

Aliitaka serikali kuruhusu mapema waangalizi kutoka nje ambao watafanya kazi ya kuona kama utaratibu mzima wa uchaguzi unazingatia vigezo vya haki na huru.



Agathon Rwasa

Umoja wa Mataifa umeonya kwamba ukiukwaji wa haki za binadamu unaweza kuongezeka tena kabla ya uchaguzi.

### KATIBA KUBADILISHWA

Mwezi uliopita, bunge la nchi hiyo liliidhinisha kwa nguvu muswada wa kuwapa nafasi ya marais wastaafu kupata mafao ikiwamo nyumba ya kifahari na malipo ya dola za Marekani 500,000.

Kiasi kinaelezwa na wachambuzi mbalimbali kuwa ni kikubwa ukilinganisha na mapato halisi ya Burundi ambayo asilimia 65 wananchi wake wanaishi katika umaskini.

Rwasa amejitokeza kupinga muswada huo akidai utakuwa mzigo kwa wananchi wa Burundi ambao wengi wanaishi chini ya dola moja.

### NANI AGATHON RWASA

Agathon Rwasa alizaliwa Januari 10 mwaka 1964 katika Mkoa wa Ngozi kaskazini mwa nchi ya Burundi.

Rwasa ambaye ni baba wa watoto saba, amesoma shule ya msingi na sekondari katika eneo hilo. Alipofika miaka 20 alichaguliwa kuwa kiongozi wa wa jumuiya ya vijana.

Baada ya kuhitimu kutoka Chuo Kikuu cha Burundi, alitakiwa kufanya kazi na serikali kama walivyokuwa wasomi wengine wengi wa Kihutu katoka mkoa huo.

Wakati wa kupambana na siasa za ukabila, kiongozi huyo alijiunga na chama cha FNL ambacho kilijihusisha na mapambano ya msituni, haraka alianza kuaminika na kupanda madaraka hadi kuwa kiongozi wa chama hicho.

Hata hivyo FNL kilishtumiwa kwa kutumia watoto kama wanajeshi na mauaji ya kikatili kwa wanawake na watoto.

Mwaka 2010, Rwasa aliendа mafichoni, akidai kuwindwa kwa tuhuma za kuhusika katika machafuko hata hivyo serikali ilikanusha.

Mnamo Julai 2015, alichaguliwa kuwa Spika wa Bunge la Burundi.

## HABARI KIMATAIFA

# Urusi yajaribu kumsaidia Trump

**WASHINGTON,** Marekani

KITENGO cha ujasusi cha Marekani kimeonya kwamba Urusi inajaribu tena kumsaidia rais Donald Trump kuchaguliwa katika uchaguzi wa mwezi Novemba mwaka huu.

Kulingana na ripoti za vyombo vya habari nchini Marekani, taarifa hiyo imefichuka baada ya mkutano wa faragha uliofanywa na kamati ya kijasusi Februari 13 mwaka huu.

Hata hivyo, taarifa hiyo ilimkasirisha Rais Donald Trump akilalamika kwamba wanachama wa Democrats watatumia habari hiyo kumchafua.

**Kiongozi huyo anakumbuka mashtaka aliyofunguliwa na bunge la uwakilishi nchini humo kwa utumiaji mbaya wa mamlaka na kuzuia bunge kufanya kazi yake.**

Trump (pichani) alimbadilisha Ofisa Mkuu wa Ujasusi, Joseph Maguire, siku ya Alhamisi. Gazeti la The New York Times liliripoti kwamba Trump alikerwa kwamba Adam Schiff, mwanachama wa Democrat aliyeongoza kesi dhidi yake alikuwa katika mkutano huo.

Kiongozi huyo anakumbuka mashtaka aliyofunguliwa na bunge la uwakilishi nchini humo kwa utumiaji mbaya wa mamlaka na kuzuia bunge kufanya kazi yake.

Aliondolewa makosa baada ya kesi hiyo iliochukua takriban wiki mbili katika bunge la seneti linalodhibitiwa na wanachama wengi wa Republican.

Wakati wa mkutano huo , wafuasi wa Trump walimtetea rais huyo kuwa amechukuwa msimamo mkali na kwamba ushirikiano wake na mataifa ya Ulaya umeimarishwa.

Schiff baadaye alituma ujumbe wa twitter kwamba Trump alikuwa akiingilia kati ugawaji wa habari kati ya kitengo cha ujasusi cha Marekni na bunge la Congress kuhusu uingiliaji wa kigeni katika uchaguzi mkuu.



Maofisa wawili wa utawala wa rais Trump waliambia gazeti la New York Times, kwamba Maguire alibadilishwa muda mfupi baada ya mkutano huo uliojaa utata.

Maofisa wa kitengo cha ujasusisi nchini Marekani wanasema kwamba Urusi iliingilia uchaguzi mkuu wa urais 2016, ili kupiga jeki kampeni ya rais Trump na kuibua malalamiko katika mchakato mzima wa uchaguzi nchini Marekani.

Wanachama wa Democrats walimkosoa rais kwa kumchagua Grenell ambaye awali alipinga kiwango cha Urusi kuingilia uchaguzi uliopita. **BBC**

## Waziri mkuu Lesotho akimbia nchi yake

**MASERU,** Lesotho

WAZIRI mkuu wa Lesotho Thomas Thabane, ameshindwa kufika mbele ya mahakama kujibu mashtaka ya kumuua mkewe wa zamani mwaka 2017.

Mtoto wa Thabane ambaye pia ni mshauri wake, alisema baba yake huyo mwenye umri wa miaka 80 amekwenda kupata matibabu katika taifa jirani la Afrika kusini.

Mkewe wa sasa Maesaiah Thabane, ameshtakiwa na mauaji hayo. Thabane atakuwa kiongozi wa kwanza wa Afrika kushtakiwa kwa mauaji akiwa ofisini.


Hata hivyo, kiongozi huyo hajatoa tamko lolote kuhusu madai hayo. Maofisa wa polisi siku ya Alhamisi walisema kwamba atashtakiwa kwa mauaji na jana siku ya Ijumaa alitarajiwa kufikishwa mahakamani, kwa mujibu wa Reuters.

Lakini jana hakwenda mahakamani , badala yake alisafiri hadi Afrika kusini kwa ajili ya matibabu , alisema katibu wake Thabo Thakalekoala. Lakini naibu kamishna wa polisi Paseka Mokete, aliwaambia waandishi habari kwamba alikuwa hajui kuhusu aliko Thabane , lakini alisema iwapo angekuwa nje ya taifa akipokea matibabu basi wangelazimika kusubiri hadi arudi.

Mkewe wa kwanza wa Thabane, 58. alipigwa risasi katika mji mkuu wa Maseru, siku mbili kabla ya kuapishwa kuwa waziri mkuu 2017. Lipolelo alipigwa risasi akiwa kandokando ya barabara alipokuwa akirudi nyumbani kutoka katika kijiji kidogo kandokando ya mji mkuu wa Maseru.

Wakati huo wawili hao walikuwa na harakati ya kupeana talaka, wakati huo, waziri mkuu alikuwa akiishi na Maesaiah, mwenye umri wa miaka 42 kama mkewe.

Lipolelo alieshinda kesi ya kutambuliwa kama mke wa kwanza wa waziri mkuu badala ya Maesaiah. **BBC**




Wanachama wa Democrat wanaowania nafasi ya nafasi ya urais, Seneta Elizabeth Warren na Bernie Sanders (kulia), wakizungumza jambo wakati wa mapumziko baada ya mdahalo katika eneo la Paris, Las Vegas juzi. **PICHA: AFP**

## Rwanda yapinga uchunguzi kifo cha Mihigo

**KIGALI,** Rwanda

RWANDA imepinga shinikizo kutoka kwa mashirika ya kutetea haki za binadamu ya kutaka uchunguzi huru kuhusu kifo cha msanii maarufu wa muziki wa kiinjili Kizito Mihigo.

Kizito (pichani) alikutwa amefariki katika kituo cha polisi Jumatatu ya wiki hii baada ya kujinyonga.

Kifo chake kilitokea siku tatu baada ya kukamatwa karibu na mpaka wa Burundi, polisi wakimtuhumu kwa jaribio la kutaka kutoroka nchi na kujiunga na kundi la waasi wanaopigana dhidi ya serikali ya Rwanda.

Mihigo alipigwa marufuku kuondoka nchini Rwanda kutokana kuwa na mashitaka yanayomkabili.

Msemaji wa shirika la upelelezi la Rwanda, Marie Michelle Umuhoza, ameiambia BBC kwamba Rwanda ni nchi huru inayojitawala na ambayo ina uwezo wa kuchunguza kitu chochote.

Mashirika ya kutetea haki za binadamu ya Human Rights Watch, Amnesty International na Commonwealth Human Rights Initiative, yameshinikiza kufanyika kwa uchunguzi huru kubaini mazingira yaliyosababisha kifo cha mwanamuziki huyo aliyekuwa na miaka 38.

Ofisa wa Human Rights Watch ameiambia BBC kwamba uchunguzi huru utaangalia kamera za siri katika eneo ambalo msanii huyo alikuwa anazuiliwa.

Lakini Umuhoza amesema Rwanda tayari inafanya uchunguzi kuhusu kifo chake.



"Sioni haja ya kufanyika kwa uchunguzi huru, katika nchi huru", alisema.

Pia alisema kwamba familia ya msanii huyo iko huru kumzika. Baadhi ya marafiki zake na wanaharakati wa Rwanda wanaoishi nje ya nchi wametilia shaka mazingira ya kifo chake.

Wamesema kwamba mwanamuziki huyo hakutaka kujiunga na kundi la waasi nchini Burundi na kwamba alitaka kwenda Ubelgiji ambapo alikuwa akiishi.

Pia wanaamini kwamba hakujiua katika kituo cha polisi alipokuwa anazuiliwa na kwamba huenda aliuawa. **BBC**

# HADITHI


ILISEMWA hapo zamani kuwa dunia inaharibiwa na vitu viwili tu. Mapenzi na mali. Vitu hivi vinaweza kumfanya binadamu aende popote. Afanye chochote kile ili awenavyo, wengine wanakwenda mbali zaidi mpaka ikiwezekana hata kutoa uhai wa wenzao.

Shani, binti wa kitajiri anapitia kwenye mikasa mikubwa mizito ya kupotezwa kwa wazazi wake na kumsababishia ukiwa na mawazo tele. Wakati ikionekana binti huyo pekee kwa wazazi wake akielekea kurithi utajiri wa wazazi wake, kiu ya damu inaanza kuwaingia baadhi ya ndugu za wazazi wake ili apoteze maisha, wao waweze kumiliki mali hizo.

Hapo ndipo uhai wa Shani unapokuwa matatani na patashika nguo kuchanika inapoanza. Fuatilia mkasa huu kuburudisha, kuelimisha na kusikitisha.

# MAUAJI HARUSINI-1

**Mtunzi anapatikana (0716 350534)**




**Na Adam Fungamwango**

"Sitaki mtu yoyote akosee. Ninayetaka wafe wote wawili, bwana harusi." Sauti nzito ilisikika kwenye kikao hicho.

Kila mmoja alikuwa kimya akimsikiliza kwa makini.

"Sitaki nisikie sijui mmoja hakufa, amelazwa hospitalini, amejeruhiwa, hiyo itakuwa ni mbaya sana na itakuwa ni sawa na mpango huu kuvurugika, lakini pia kuwa kwenye hatihati ya kutiwa mbaoni." Alisema akiwaangalia wenzake wanne walio kwenye makocha kwa makini akiwa amekunja sura.

"Sawa bosi tumekuelewa na kwangu mimi naahidi nitatekeleza maagizo yote ninayotakiwa nitekeleze." Ilikuwa ni sauti ya kijana mmoja asiyezidi miaka 30 hivi.

Alikuwa amekaa kwa utulivu, kana kwamba inapangwa mipango ya sherehe za harusi na si kwenda kuua.

"Nataka nchi nzima kama si jiji zima la Dar es Salaam lisisimke. Lirindime. Najua baada ya tukio polisi watasambaa huku na huko kutafuta watuhumiwa na chanzo. Lakini kwa namna mipango tulivyopanga kimadhubuti, hakuna atakayeambua kitu." Bosi alizidi kusisitiza na akatabasamu, tabasamu ambalo halikuwa halisi na akaongeza.

**Sitaki nisikie sijui mmoja hakufa, amelazwa hospitalini, amejeruhiwa, hiyo itakuwa ni mbaya sana na itakuwa ni sawa na mpango huu kuvurugika, lakini pia kuwa kwenye hatihati ya kutiwa mbaoni.**

"Sijawahi kushindwa mimi katika opeshereni zangu."

"Bosi mimi nina swali au ombi." Mmoja wa waliokuwa kwenye kikao hicho cha faragha alivunja ukimya wa muda mrefu.

"Uliza bwana Tamim." Bosi alimpa ruhusa.

"Mimi ndiyo nitakayefyatua risasi ya kumuua bwana harusi na bibi harusi, si ndiyo?"

"Ndiyo maana yake."

"Sasa hiyo milioni kumi kwangu ni ndogo sana."

"Kivipi, sijakuelewa."

"Hiyo kwangu ni shombo tupu. Siwezi kuua mtu kwa pesa hiyo. Pamoja na kwamba nina madhambi mengi ya kuua binadamu lukuki, lakini hata siku moja sitoweza kujirahisisha kuua binadamu kwa kiasi hicho. Waswahili wanasema ukitaka kula nguruwe, kula aliyenona." Alisema Tamim kwa kujiamini na kwa utulivu mkubwa.

"Wewe unahitaji ngapi?"

"Nahitaji mzigo wa shilingi milioni 30 uwekwe mezani, ndiyo niinue mguu wangu kwenda kufanya mauaji."

"Vizuri Tamim. Najua wewe ni mtaalam wa kazi hii na umeifanya kwa miaka mingi, lakini kiasi hicho ni kikubwa sana punguza kidogo bwana, kwa sababu inawezekana kabisa huu unaweza ukawa si mwisho, tunaweza kupata dili lingine kama hili, nikakupa kazi kwa mara nyingine tena." Bosi aliomba bei ipunguzwe kidogo.

"Basi hebu nipe milioni 20, mimi nitakufanyia kazi yako vizuri sana, hakuna atakayekuwa hai siku hiyo wote wawili, hakuhakikishia."

"Haidhuru, nitakupa hiyo 20, lakini usiniangushe."

"Asante bosi nashukuru."

"Enhee, wengine tumeelewana? Kuna mtu ana swali?"

"Ndiyo bosi, ni hivi, hawa maharusi wanatakiwa wauawe kabla au baada ya kufunga ndoa?"

Kilifuatia kicheko kikali kutoka kwa bosi.

"Bwana Michael umeshawahi kuoa au kwenda kwenye harusi yoyote ile iwe ya Kikristo, Kiislam au ya Kimila?"

Hakukuwa na jibu lolote kutoka kwa aliyeuliza swali.

"Huwezi kukamata au kuwaua bwana harusi na bibi harusi kwa pamoja, kabla hawajafunga ndoa kwa sababu kwa taratibu za dini zote na hata za kimila, maharusi wanakuwa pamoja baada ya ndoa kufungwa, unasikia?." Alisisitiza na kuonekana kama mwalimu anayewafundisha wanafunzi wake.

"Kabla hawajafunga ndoa huwa hawawi pamoja. Kila mmoja anatoka kwake na wanakutania Kanisani. Kwa Waislamu wanakutania Msikitini, au bwana harusi anatoka nyumbani wake na ndugu zake, jamaa na marafiki na kwenda kwao mwanamke na baada ya hapo ndipo anarejea na mkewe. Sasa kwenye huu mpango wetu, labda kama tungetaka mmoja tu ndiyo afe, lakini kwa sababu wote wawili ni kwamba, lazima wawe wameshafunga ndoa ambayo itawapa fursa ya kuambatana wote wawili, na hiyo inampa fursa hata muuaji bwana Tamim kutokuwa na kazi ngumu. Maharusi hawa wanafunga ndoa ya Kanisani." Bado alizidi kusisitiza bosi.

"Sawa Bosi, lakini hapa ni lazima tukubaliane, eneo sahihi la kufanya mauaji ni wapi? Wakati wanatoka Kanisani?

Njiani wakati wapo kwenye gari, au nyumbani kwa bwana harusi wakati wanawasili?" Mmoja aliyekuwa kwenye kikao hicho akauliza.

"Mimi nadhani swali hilo tungemtupia Tamim alijibu kwa sababu mimi binafsi ninachohitaji bwana harusi na bibi harusi wauawe tu basi. Sijali wauawe vipi au wauawe wapi. Ninachohitaji wasiwepo kwenye uso wa dunia." Aliunguruma bosi.

"Mimi nadhani, sehemu ambayo itakuwa rahisi sana kuwaua wote wawili ni pale watakapokuwa wanashuka kwenye gari lao, wakipokelewa na ndugu zao, kuelekea sehemu ambayo wameitenga kwa sherehe au kuelekea kuingia nyumbani kwao. Hiyo ni sehemu ambayo mara nyingi inakuwa si tulivu, kunakuwa na pilikapilika na shamrashamra ya ngoma na mbwembwe nyingi, kwa hiyo kunakuwa hakuna utulivu, au watu wanaofuatilia jambo lingine zaidi ya kuwaona maharusi." Tamim alitoa msimamo wake kutokana na uzoefu wa kazi yake hiyo kutokana na kuifanya kazi hiyo ya kuua watu kwenye sehemu tofauti na mazingira tofauti pia.

"Bwana Tofiki, hakikisha gari letu linakuwa moja kati ya magari ya mbele kwenye msafara wa harusi ili kazi yetu isiwe ngumu sana. Na hakikisha, wakati muda ukiwadia wa kufanya mauaji, basi hakikisha gari liwe limeshatoka eneo la magari mengine yaliyo kwenye msafara na kukaa kwenye eneo sahihi pekee ambalo mambo yakishamalizika, basi gari haraka sana linaondoka na kwa ninavyokujua kuwa ni mtaalam wa kuendesha magari kwa kasi, hata wakifukuza na pikipiki ya polisi hawawezi kutupata."

"Bwana Tamim, kila mtu na utaalamu wake, wewe ukishamaliza kula vichwa, hayo mambo ya kutambaa na gari niachie mimi." Tofiki, ambaye mtaalam wa kuendesha gari kwa kasi, na alishawahi kuwa mshindi wa mbio za magari miaka mitatu iliyopita, alijisifu mbele ya wenzake.

**Itaendelea Jumamosi**

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## MATANGAZO MCHANGANYIKO

**NYUMBA INAUZWA MIL 70 ARUSHA NGULELO:**, SELF VYUMBA 3 KIMOJA MASTER, SITTING, JIKO NA STORE, INA UMEME âNA MAJI INAFAA KUISHI, FINISHING NA FENSI UNAIMALIZIA. MWENYE NYUMBA **0757 804 970**

NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI

BIDHAA YAKO

KWA BEI NAFUU SANA

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**NIDA TEXTILE MILLS (T) LIMITED** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA SEMI TRAILER YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 943 CKX.** CHASSIS NO. **AMT011025512.** KWA YOYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI : **KAH/ /RB/ 68/2020.**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**PRONTO HAULIERS TANZANIA LIMITED** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA SCANIA YENYE NAMBA ZA USAJILI **T534CGR CHASSIS NO 4508984** NA ENGINE **NO 6213805** KWA YOYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI

**TAARIFA YA POLISI**

**KAH/ /RB/ 69/2020**

215641402

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MARIAM ATHUMANI ALLY** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 640 CTU NISSAN CARAVAN.** Chassis namba **24051035.** Engine namba **td27306531.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:

**TAN/TAN/RB/159546/2020.**

215641502

**UTAMBULISHO WA USIMAMIZI WA USIMAMIZI WA MIRATHI**

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**

**TANGA**

**SHAURI NA.6/2019**

**MAOMBI YA BARUA YA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU KARL RUDDY MULLER**

**NA**

**CHRISTINE MWALONGO MULLER....................MWOMBAJI**

**FOMU 58**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(KANUNI YA 75)**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na haki katika Mirathi ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia shauri hili katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa barua ya usimamizi wa mirathi kwa muombaji aliyetajwa hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 10/03/2020
Imewasilishwa Tanga leo tarehe 12/02/2020

NAIBU MSAJILI

215640702

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

## Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe

www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi**

**Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# SOLSKJAER ALALAMIKIA UWANJA, MPIRA MAN UNITED IKISHIKWA




**MANCHESTER,** England

OLE Gunnar Solskjaer amedai kwamba hali ya hewa, ubovu wa uwanja na mpira uliotumika kwenye mchezo huo wa Ligi ya Europa vilichangia Manchester United kupata sare dhidi ya Club Brugge.

Anthony Martial alifunga bao kusawazisha lile la Emmanuel Bonaventure Dennis na kuwapa United faida ya bao la ugenini kuelekea mchezo wa marudiano pale kwenye dimba la Old Trafford. Baada ya mchezo huo, Solskjaer alisema hali ya uwanja na mpira ndio ilikuwa sababu ya sare hiyo.

"Ulikuwa mchezo mgumu dhidi ya timu iliyojipanga," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Sidhani kama ulikuwa mchezo mzuri ambao watu waliushuhudia. "Hali ya hewa, hali ya uwanja na mpira zilifanya mchezo kuwa mgumu zaidi kwa upande wetu.

# Barca yalalamikiwa rafu usajili wa Braithwaite




**BARCELONA,** Hispania

RAIS wa Barcelona, Josep Maria Bartomeu, ametetea uamuzi wa klabu yake kumsajili Martin Braithwaite, lakini alibainisha kuwa Leganes wanahaki ya kuona hawajatendewa haki kwa usajili huo.

Mabingwa hao wa Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, walithibitisha Alhamisi kumsajili mshambuliaji huyo kwa ada iliyowekwa kwenye kipengele cha mkataba wake kama akitaka kuondoka ya euro milioni 18.

Barca walipewa ruhusa ya kumsajili Braithwaite wakati huu ambapo dirisha la usajili limefungwa baada ya kuwapoteza Luis Suarez na Ousmane Dembele ambao watakuwa nje ya uwanja kwa muda mrefu baada ya kuumia.

Leganes ambao wanasuasua kwenye Ligi Kuu ya Hispana, LaLiga, hawakuruhusiwa kusajili mchezaji wa kuziba pengo la mshambuliaji huyo, huku Mkurugenzi mkuu wa klabu hiyo, Martin Ortega akilishutumu Shirikisho la Soka la Hispania.

Ortega alilishutumu shirikisho hilo kwa kuwasababishia "matatizo" Leganes na ametaka sheria hiyo kurekebishwa.

Akizungumza wakati wa kumtambulisha Braithwaite Alhamisi, Bartomeu alikubali kwamba sheria hiyo inatakiwa kuangaliwa upya.

# Arteta aimwagia sifa Arsenal, Saka

**LONDON,** England

MIKEL Arteta ameisifia timu yake ya Arsenal kwa kuwa na moyo wa kujituma, wakati wakiibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Olympiacos kwenye mchezo wa Ligi ya Europa juzi, Alhamisi huku pia akikikubali kiwango cha kinda, Bukayo Saka.

Bao la Alexandre Lacazette la dakika ya 81, liliwawezesha "Washikabunduki' hao wa London kuwa na nafasi ya kusonga mbele na kujirahisishia mchezo wa pili wa hatua hiyo ya timu 32, wakati watakaporudiana katika dimba la Emirates wiki ijayo.

Kilikuwa kiwango cha kuvutia kwa Arsenal, huku mabeki Shkodran Mustafi na Sokratis Papastathopoulos mwishoni waliumia na kutibiwa katika dimba la Georgios Karaiskakis.

Arsenal sasa haijapoteza katika mechi zake tisa zilizopita katika mashindano yote, huku Arteta akisifia morali ya timu yake iliyoonyesha nchini Ugiriki.

"Tunakwenda siku kwa siku na mchezo kwa mchezo kwa sababu tunavyoendelea mbele kunakuwa na mambo mengi na ndio maana nataka timu iimarike," alisema Arteta akiiambia BT Sport.

"Wakati huo huo, wanacheza kwa kujituma na kwa moyo mmoja – na namna wanavyoshambulia, tuna wachezaji watatu ambao ni majeruhi, naamini watarudi dimbani muda si mrefu."

Bao hilo la Arsenal ambalo lilitengenezwa na winga kijana, Saka ambapo alifikisha pasi za mwisho tano msimu huu kwenye Europa – ikiwa nyingi zaidi kuliko mchezaji yoyote, licha ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 18 kucheza beki ya kushoto.

Na Arteta anaamini Saka yuko kwenye kiwango bora zaidi kwa sasa na anazidi kuimarika siku hadi siku.

"Nafurahishwa sana na kiwango chake, tunajaribu kumuweka sehemu ambayo anaweza kuzungukwa na wachezaji wengi na yeye si beki wa pembeni," alisema Arteta.



HABARI MICHEZO

# Willian kubobea London hata akiachwa Chelsea

**LONDON,** England

WILLIAN amedokeza kwamba ataangalia uwezekano wa kutafuta klabu nyingine ya jijini London ili kuichezea kama Chelsea watashindwa kumuongezea mkataba wake, akidai atalazimika kubakia kwenye mji huo mkuu wa England kwa sababu za kifamilia.

Winga huyo wa kimataifa wa Brazil, Willian, amekuwa pale Chelsea tangu mwaka 2013, ambako alijiunga na timu hiyo akitokea Anzhi Makhachkala ya Urusi na amekuwa akicheza kikosi cha kwanza mara kwa mara katika maisha yake hapo Stamford Bridge.

Willian amecheza mechi zote kasoro moja kati ya 26 za Ligi Kuu kwa Chelsea msimu huu, licha ya kushutumiwa na mashabiki wengi, Frank Lampard, ameendelea kumuamini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31.

Alidai Desemba mwaka jana kwamba, mazungumzo ya mkataba mpya yamefanyika na anaweza kuongezewa mwishoni mwa msimu, lakini hadi sasa makubaliano yao hayajawekwa wazi.

Kutokana na usajili wa Hakim Ziyech kutoka Ajax ambaye atatua hapo Julai mwaka huu kunaiweka shaka nafasi ya Willian.

Lakini Willian mwenyewe amesema anapanga kubaki jijini Londo na hata kama Chelsea hawatamuongezea mkataba.

"Nimeichezea Chelsea kwa zaidi ya miaka sita sasa, kwa ukweli kabisa naweza kusema nina furaha kuwa hapa.

"Kama ukimuuliza mke wangu endapo anataka kuondoka London, atasema hapana. Binti zangu nao hivyo hivyo. Bila shaka Brazil ni Brazil, sawa? Kule ni nyumbani kwetu na tuna tamaduni zetu.






# JUVENTUS WAPANGA KUMSAJILI JESUS

**TURIN,** Italia

MSHAMBULIAJI wa Manchester City, Gabriel Jesus, ameripotiwa kwamba anatakiwa na klabu ya Ligi Kuu ya Italia, Serie A, Juventus.

Jesus mwenye umri wa miaka 22, amekuwa kwenye wakati mgumu wa kupata namba kikosi cha kwanza msimu huu tangu alipotua hapo City akitokea Palmeiras mwanzoni mwa mwaka 2017.

Na Juve imeripotiwa inajiandaa kumsajili mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil ili akatue kule kwenye viunga vya Turin.

Juventus wanataka kulipa kiasi cha pauni milioni 58.5 kwa Jesus ili wamsajili, kwa mujibu wa gazeti la The Sun.

Ripoti hiyo inadai kwamba, mabingwa hao wa Serie A, pia wanamtaka Mauro Icardi, ambaye anacheza kwa mkopo kule Paris Saint-Germain akitokea Inter Milan.

Jesus amefunga mabao 36 katika mechi 90 za Ligi Kuu ya England kwa City, lakini 48 tu ndio alianza.

# Conte: Eriksen bado hajawa fiti

**SOFIA,** Bulgaria

CHRISTIAN Eriksen bado hajafikia kiwango chake baada ya kujiunga na Inter Milan kutoka Tottenham, kwa mujibu wa kocha, Antonio Conte.

Eriksen, ambaye alisajiliwa na klabu hiyo ya Ligi Kuu ya Italia, Serie A, wakati wa dirisha la Januari, alifunga bao lake la kwanza kwa Inter wakati wakiibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Ludogorets kwenye mchezo wa kuwania Kombe la Ligi ya Europa hatua ya timu 32.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Denmark alifunga bao hilo kwa shuti kali na pia shuti lake jingine liligonga mwamba kabla ya penalti ya dakika za majeruhi iliyopigwa na Romelu Lukaku kuwahakikishia ushindi Nerazzurri hao kuelekea kwenye mchezo wa marudiano utakaopigwa mjini Milan.

Hata hivyo, Conte anahisi bado kuna mengi yanakuja kutoka kwa Eriksen.

"Nina furaha naye, bao mara zote linampa kujiamini," alisema Conte akiiambia Sky Sport Italia baada ya Inter kupata ushindi huo nchini Bulgaria.

"Christian anahitaji kujifua zaidi ili awe fiti, bado hajawa bora kama alivyokuwa kule Tottenham.

"Anaweza kufanya zaidi kwa kile alichokionyesha leo [juzi], lakini tuna furaha kubwa kwa sababu tunajua anaweza kutupa mazuri mengi zaidi."



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# MESSI SASA AIWEKA MAN CITY KAPUNI

●●● Ligi ya Mabingwa inavutia sana, miaka miwili bila kucheza ni ngumu, wachezaji wengi...

**MANCHESTER,** England

MATUMAINI ya Manchester City kusajili majina makubwa katika soka, akiwamo Lionel Messi, kwa sasa yataathiriwa zaidi kama kifungo cha kushiriki Ligi ya Mabingwa Ulaya hakitaondolewa na tayari nyota huyo wa Argentina naye ameiweka kapuni klabu hiyo kwa kueleza uwezekano wa mastaa kuondoka hapo Etihad.

**Klabu hiyo imekata rufaa kuhusu kifungo hicho cha kutoshiriki michuano ya Ulaya kwa msimu wa 2020/21 na 2021/22.**

City inaamini inaweza kupindua kifungo hicho, lakini itahitajika juhudi kubwa kuweza kuishawishi Mahakama ya Usuluhishi ya Michezo, CAS.

Kifungo cha misimu miwili kitaondoa matumaini ya kuendeleza mafanikio yao ya sasa huku kukiwa na uwezekano wa wachezaji wao kuondoka. Na Man City sasa inaweza kusema kwaheri kuhusu matumaini yao yoyote ya kumsajili Messi.

Nyota huyo wa Barcelona amekuwa akihusishwa na kutua Etihad na tetesi hizo zikizidi kufuatia Messi kutibuana na bodi ya Barcelona. Messi ni wazi atazingatia klabu inayompa nafasi ya kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya na alizungumza kuhusu City wakati akifanya mahojiano na gazeti la Mundo Deportivo.

Mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Argentina, alifunguka kuwa wachezaji wa City wanaweza kutazama kuondoka na kisha akaenda mbali kwa kusema watachoshwa na miaka miwili bila kushiriki michuano mikubwa ya soka ya Ulaya.

"Inashangaza kwa sababu hakuna yeyote aliyedhania kitu kama hicho kinaweza kutokea," Messi alisema.

"Paris [Saint-Germain] ililipa faini ama sijui namna lilivyokwenda. Kama mwishoni City haitacheza Ligi ya Mabingwa kwa namna ilivyo, na wachezaji, klabu na hela zilizotumia, itakuwa dhaifu.

"Kuna wachezaji wengi watatazama kuondoka ama pengine hapana. Ligi ya Mabingwa inavutia sana, hivyo miaka miwili bila kucheza inachosha."

## ZISIKUPITE

### KLOPP AWAKERA ATLETICO

WACHEZAJI wa Atletico Madrid, walikuwa na hasira na madai ya kocha wa Liverpool, Jurgen Klopp, baada ya kuwafunga 'Wekundu' hao kwa bao 1-0 kwenye mechi ya mkondo wa kwanza wa Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16-bora, na wanadhani Mjerumani huyo alipaswa kuzingatia zaidi timu yake. ***(ESPN)***

### BARCA, CITY KWA MILAN

MANCHESTER City na Barcelona watapaswa kulipa zaidi ya pauni milioni 75 ili kumpata beki wa Inter Milan, Mslovakia Milan Skriniar, 25. ***(Calciomercato)***

### ARSENAL YAMKOMALIA TAH

ARSENAL inazingatia uwezekano wa kulipa pauni milioni 34 zinazohitajika ili kuvunja mkataba wa beki wa Bayer Leverkusen na Ujerumani, Jonathan Tah, 24. ***(Bild - in German)***

### ALONSO DADO LULU INTER

BEKI wa pembeni wa Hispania, Marcos Alonso, bado anawindwa na Inter Milan - lakini Chelsea inajiandaa kupandisha dau la kumuuza mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29. ***(Calicomercato - in Italian)***

### HODGSON KUFUNGWA PALACE

MWENYEKITI wa Crystal Palace, Steve Parish, amesema anaamini atambakisha kocha Roy Hodgson klabuni hapo baada ya kumpa ofa ya mkataba mpya. ***(Sky Sports)***

### WILLIAN HATAONDOKA LONDON

WINGA wa Chelsea, Mbrazil Willian, 31, atamaliza mkataba wake mwishoni mwa msimu, lakini amesema hana mpango wa kuiondoa familia yake katika makazi yake hapo London. ***(Mail)***

### SOLSKJAER AMTAJA ERIKSEN

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, alikuwa tayari kumsajili Christian Eriksen kabla ya kiungo huyo Mdenmark kuondoka Tottenham na kujiunga na Inter Milan mwezi uliopita. ***(Manchester Evening News)***

### BRAITHWAITE ALETA SHIDA

TIMU iliyopo katika wakati mgumu kwenye La Liga, Leganes wamekasirika Barcelona kuruhusiwa kumsajili mshambuliaji wao Mdenmark Martin Braithwaite, 28, baada ya dirisha kufungwa na inatumai itapewa nafasi kama hiyo ya kusajili straika. ***(AS)***

### JUVE, INTER KWA PALMIERI

JUVENTUS na Inter zinavutiwa kumsajili beki wa pembeni wa Chelsea, Emerson Palmieri lakini bado haizijatoa ofa rasmi kwa Mtaliano huyo mwenye umri wa miaka 25, kwa mujibu wa wakala wake. ***(Goal.com)***

### CAMAVINGA AIPAGAWISHA REAL

REAL Madrid inamfuatilia mchezaji anayeelezwa kuwa na kipaji cha hali ya juu, kiungo wa Rennes na Ufaransa U-21, Eduardo Camavinga, 17. ***(Marca)***

### FRUCHTL ALIVOITOLEA NJE LIVER

KIPA wa Bayern Munich, Mjerumani Christian Fruchtl, 20, alikataa kujiunga na Liverpool mwaka jana kwa sababu hakujiandaa kuwa kipa wa akiba. ***(Sport1, via Mirror)***

HABARI MICHEZO

## Harerimana ageukia saikolojia KMC

Na Saada Akida

BAADA ya kushindwa kupata matokeo mfululizo, Kocha Mkuu wa KMC, Haruna Harerimana, amesema kwa sasa anawajenga kisaikolojia wachezaji wake ili kuwaondolea hali ya usahaulifu inayowaandama hadi kuchangia kusahau maelekezo yake wanapokuwa dimbani.

KMC kwa sasa ipo nafasi ya 17 ikiwa na pointi 21 baada ya kucheza mechi 23, na Jumanne wiki hii ilikubali kichapo cha mabao 2-1 dhidi ya Namungo FC kwenye mchezo uliochezwa Uwanja wa Majaliwa mkoani Lindi.

Na wakati leo Jumamosi KMC ikijiandaa kuivaa Ndanda FC katika Uwanja wa Nangwanda Sijaona mkoani Mtwara, Kocha huyo ameliambia Nipashe kuwa, ameamua kugeukia kufanyia kazi mapungufu ya kikosi chake hususan kuanza kwa kuwajenga wachezaji kisaikolojia.

Alisema darasa hilo linakwenda sambamba na kuhakikisha wachezaji wake wanazingatia mbinu anazowapa katika mazoezi kwa ajili ya kupambana kutafuta alama tatu.

"Wachezaji wangu ninawapa maelekezo ya kufanya kipindi cha kwanza, tatizo wakiingia uwanjani wanasahau na kufanya mambo mengine, jambo hilo linanifanya nikirudi mapumziko kuanza upya," alisema Haruna.

Aliongeza: "Hali ya timu haiko katika nafasi nzuri inatulazimu tutafute pointi, wakati huo huo tusifungwe, hivyo umakini unahitajika zaidi ili kujiondoa katika nafasi ya kushuka daraja."

## Mabadiliko mbio za 'Relay' Taifa

Na Mwandishi Wetu

MASHINDANO ya Mbio za Kupokezana Vijiti 'Relay' Taifa yaliyokuwa yafanyike leo, Jumamosi Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam, sasa yamesogezwa mbele hadi kesho Jumapili, imeelezwa.

Kwa mujibu wa Taarifa iliyotolewa na jana Msemaji wa Shirikisho la Riadha Tanzania (RT), Tullo Chambo, sababu ya kusogezwa mbele kwa siku moja mashindano hayo, ni ili kutoa nafasi kwa wachezaji kufika jijini Dar es Salaam, baada ya baadhi yao kukabiliwa na changamoto ya usafiri.

Alisema mashindano hayo yatashirikisha mbio za mita 100X4 na 400X4 yakishirikisha wanariadha kutoka mikoa tisa waliofikia viwango maalumu vilivyowekwa na Kamati ya Ufundi ya RT.

"Mashindano haya, yanafanyika baada ya mikoa mbalimbali kuendesha mashindano 'Trials' na wale wanariadha waliofikia viwango vilivyowekwa na Kamati ya Ufundi ya RT, ndio wanakutana katika fainali Jumapili.

"Tunaamini viongozi wa mikoa wamezingatia viwango tulivyotoa na hakuna udanganyifu, hivyo tunategemea ushindani utakuwa mkubwa sana na tutapata timu nzuri," ilieleza taarifa hiyo.

# TWIGA STARS YATOLEA JICHO UBINGWA UNAF

Na Somoe Ng'itu, TUNISIA

TIMU ya Soka ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars), inatarajia kuwakabili wenyeji Tunisia katika mechi ya mwisho ya mashindano ya Kanda ya Kaskazini (UNAF) itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Kram jijini Tunis nchini hapa.

**Mechi hiyo itakayoanza saa 9: 15 mchana kwa saa za Afrika Mashariki itakuwa ni ya kukamilisha ratiba kwa wenyeji Tunisia yenye pointi nne, lakini Twiga Stars ambayo ina pointi sita inaweza kuibuka mabingwa endapo itapata ushindi wowote huku ikiombea Morocco ipoteze dhidi ya Algeria katika mechi ya mapema asubuhi.**

Akizungumza na Nipashe jijini hapa, Kocha Mkuu wa Twiga Stars, Bakari Shime alisema amekiandaa kikosi chake kumaliza vema katika mashindano hayo bila kuangalia matokeo ya timu nyingine.

Shime alisema kupitia mashindano hayo, wachezaji wake wameimarika na watakuwa tayari kuikabili Kenya katika mechi ya kusaka tiketi ya kushiriki fainali zijazo za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa wanawake (AWC), itakayochezwa mapema Aprili mwaka huu.

Kocha huyo alisema ameridhishwa na viwango vya wachezaji wake ambao kwa muda mrefu walikosa mechi za mashindano na anaamini matunda ya michuano hii yataonekana katika michezo inayofuata.

"Nimewaona Tunisia mara zote tatu, ninajua ubora wao, nimefanya marekebisho katika makosa tuliyofanya, naamini tutaingia na nguvu mpya katika mechi ya kesho (leo), najua wao pia watajipanga kumaliza kwa heshima," alisema Shime.

Aliongeza mechi hiyo haitakuwa nyepesi kwa kila timu kwa sababu wenyeji hawatakubali kuona wanamaliza michuano hii wakiwa mkiani.

Nahodha wa timu hiyo, Asha Rashid, alisema kila mchezaji anataka kuona wanamaliza mashindano haya kama walivyoanza.

"Tumejiandaa vizuri kwa mechi ya Tunisia, hatutaki kuondoka kinyonge, hatutarudia makosa ya mechi iliyopita, tunataka wajue tulikuja hapa kupambana kuhakikisha tunarudi nyumbani na ushindi, bado nafasi tunayo, katika mpira hatupaswi kukata tamaa, tumejipanga kushinda tu," Asha alisema.

Katika mechi ya leo, Twiga Stars itamkosa beki wake Happiness Hezron kutokana na kuonyeshwa kadi nyekundu katika mchezo uliopita dhidi ya Morocco pamoja na Annastazia Katunzi ambaye ana kadi mbili za njano.

RIADHA...



Baadhi ya wanariadha wakifanya mazoezi juzi katika Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam kwa ajili ya michuano ya wazi itakayofanyika uwanjani hapo kuwania tiketi ya kushiriki michuano ya Olimpiki nchini Japan. PICHA: JUMANNE JUMA

# *Azam FC yaihofia Namungo kwao*

Na Shufaa Lyimo

VITA ya pointi tatu kati ya wenyeji wa mechi ya leo, Namungo FC dhidi ya Azam FC imezidi kupamba moto baada ya makocha wa timu hizo kila mmoja kueleza hisia zake kuelekea mechi hiyo.

Namungo itashuka dimbani ikitaka kuendeleza furaha kwa mashabiki wake nyumbani baada ya mchezo uliopita, Jumanne kuichapa KMC FC mabao 2-1 wakati Azam ikitoka kulazimisha sare ya bao 1-1 ugenini dhidi ya Ndanda FC.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti, Kocha msaidizi wa Azam FC, Idd Cheche, alisema mchezo huo utakuwa mgumu kwa sababu wanapokutana na timu hiyo ikiwa kwao huwapa changamoto kubwa ya kushinda tofauti na wakiwa nyumbani jijini Dar es Salaam.

Alisema kikosi chake kipo tayari kwa mchezo huo wa leo isipokuwa ana wachezaji wawili majeruhi Idd Nado ambaye hakuweza kusafiri na timu baada ya kuumia kifundo cha mguu wakati walipokutana na timu ya Coastal Union, pamoja na Daniel Amoa ambaye alipata majeraha ya nyama za paja juzi walipokutana na Ndanda FC.

"Tunapokuwa ugenini dhidi ya Namungo huwa tunapata wakati mgumu, ni timu nzuri inajua kutumia vizuri nafasi inapokuwa uwanjani, kikubwa ni kujitahidi kuwajenga wachezaji kisaikolijia ili tusipoteze," alisema.

Kwa upande wa Kocha Mkuu wa Namungo FC, Hitimana Thierry, alikiri pia ugumu wa mchezo huo na kusema wataingia kwa tahadhari kubwa wakiwa na lengo la kuibuka na pointi tatu muhimu.

"Ninaendelea kuwanoa wachezaji kuhakikisha wanatumia kila mbinu kupata pointi tatu, kila mchezaji ana morali ya ushindi katika mchezo wetu huo ambao unasubiriwa na wadau mbalimbali wa soka hapa nchini, ninaomba wachezaji wazidi kujituma zaidi," alisema Hitimana.

Alisema mpaka sasa hana majeruhi hata mmoja na kila mchezaji anaendelea vizuri kiafya kuelekea mchezo huo.

Namungo ambayo imeshashuka dimbani mara 22, ipo katika nafasi ya tatu kwenye msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na pointi 40 wakati Azam FC ikiwa nafasi ya pili na alama 45 baada ya kucheza mechi 23.

# Michezo

Jumamosi Februari 22, 2020

Nipashe




Messi aiweka Man City kapuni

UKURASA 30

PANGUA...




Kipa wa Arsenal, Mjerumani Bernd Leno, akipangua hatari wakati wakishinda kwa bao 1-0 ugenini, kwenye mechi ya mkondo wa kwanza ya Europa League hatua ya 32 dhidi ya Olympiacos juzi. **HABARI UK. 28**

## Eymael kuamua Molinga, Tariq

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya kumsugulisha benchi katika mechi iliyopita, hatimaye Kocha Mkuu wa Yanga, Mbelgiji Luc Eymael, atakuwa na uwanja mpana wa kuamua kumtumia David Molinga ama Tariq Seif ambaye alizua hofu ya kuikosa Coastal Union kesho katika Uwanja wa Mkwakwani.

Katika mechi iliyopita wakati wakitoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Polisi Tanzania kwenye Uwanja wa Ushirika mjini Moshi, hiyo ikiwa ni mechi ya tatu mfululizo kutoka sare, Molinga hakucheza na safu ya ushambuliaji iliongozwa na mfungaji wa bao hilo, Tariq.

Hata hivyo, Tariq aliumia katika mchezo huo na kuzua hofu ya kukosekana kwenye mchezo dhidi ya Coastal Union kesho, lakini daktari wa Yanga, Sheck Mngazija alimeliambia Nipashe kuwa kocha ana uwanja mpana wa kupanga kikosi chake hususan safu ya ushambuliaji kufuatia straika huyo kuwa fiti kwa mchezo huo.

"Wachezaji wote wapo fiti, kuhusu Tariq Seif anaendelea vizuri kwa sababu baada ya kuumia katika mchezo na Polisi Tanzania alipata vipimo na kujiridhisha hajaumia na yupo katika programu ya mchezo wetu dhidi ya Coastal," alisema Mngazija.

Lakini Eymael, akizungumza na Nipashe jana, alisema uwezo anaonyesha Molinga wa kufunga ana imani ataifungia mabao mengi na kusaidia timu yake kufikia malengo.

"Bado nina kazi katika safu ya ushambuliaji, kwa Molinga tatizo lake anashindwa kutulia akiwa ndani ya 18 na uwanjani pia ila akipata nafasi anafunga, endapo atafanyia kazi makosa yake ana nafasi ya kufunga mabao mengi msimu huu," alisema Eymael.

# Simba kunoga tena Taifa leo

**Na Saada Akida**

## ●●● Sven aahidi burudani, kasi na mabao wakiivaa Biashara, huku akigeukia washambuliaji kwa...

WAKATI uongozi wa Klabu ya Simba ukieleza kufurahishwa na kasi mpya aliyorejea nayo nahodha wao, John Bocco, akitokea chumba cha majeruhi, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Mbelgiji Sven Vandenbroeck, amewaita mashabiki wa timu hiyo Uwanja wa Taifa kushuhudia tena burudani.

**Bocco alikosekana katika raundi ya kwanza ya Ligi Kuu Bara kutokana na kuwa majeruhi na kwenye mechi tatu zilizopita ameonekana kuwa msaada mkubwa kwa timu kuibuka na ushindi.**

Kupitia mtandao wa klabu hiyo, Simba imesifu uwezo wa Bocco kwa kueleza: "Raundi ya kwanza ya VPL tulikosa huduma yake kutokana na kuwa majeruhi. Raundi ya pili tunafurahia sana uwepo wake, mechi tatu zilizopita; mabao mawili, 'assist' pasi ya mwisho moja na penalti moja [aliyosababisha na kufungwa na Meddie Kagere]."

Hata hivyo, wakati Bocco akisifiwa kwa namna alivyorejea na kiwango bora na kuwa msaada kwa timu, Sven ameipa kazi safu yake ya ushambuliaji inayoongozwa na nahodha huyo pamoja na Kagere kuhakikisha wanaisambaratisha Biashara United leo.

Hiyo ni kutoka na mchezo uliopita dhidi ya Kagera Sugar, safu ya ushambuliaji ya 'Wekundu wa Msimbazi' hao kupoteza nafasi nyingi za kufunga na kujikuta wakiondoka na ushindi mwembamba wa bao 1-0.

Katika mazoezi ya timu hiyo yaliyofanyika uwanja wa klabu hiyo, Mo Simba Arena uliopo Bunju nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam, Sven alionekana kuikomalia zaidi safu yake ya ushambuliaji chini ya Bocco na Kagere.

Na baada ya mazoezi hayo, Sven aliliambia Nipashe kuwa kushinda kwao kunategemea idadi ya mabao ambayo yatafungwa, hivyo jukumu hilo linapaswa kutekelezwa na washambuliaji.

Alisema kila inapomaliza mechi lazima upungufu unaonekana na tayari amefanyia kazi ikiwa ni pamoja na kuwataka wachezaji wake kuendelea kujitolea kama walivyocheza kwa ari kubwa dhidi ya Kagera Sugar, lakini akiwataka kuongeza umakini langoni ili kupata idadi kubwa ya mabao wakianza na Biashara United leo.

"Nimeshatoa maelekezo kila mmoja anajua majukumu yake, kwa sasa hakuna kutafuta kisingizio cha kushindwa, hilo kwangu halipo kazi ni moja kucheza kwa juhudi na kutafuta matokeo ya idadi ya mabao mengi," alisema.

Kwa upande wake, Kocha Msaidizi wa Biashara, Omar Madenge alisema mpango mkubwa kwa timu yake ni kupambana mbele ya Simba na kupata alama tatu bila kuhofia makali ya washambuliaji wa wapinzani wao.

"Tupo tayari kupambana mbele ya safu yao ya ushambuliaji inayoongozwa na Kagere, tunajua uimara wao ulipojificha nasi hatuna mashaka, tupo vizuri na tayari kwa ajili ya mchezo huo," alisema Madenge.

Simba inayoongoza msimamo wa ligi hiyo ikiwa na alama 59, itashuka dimbani leo ikitaka kuendeleza ubabe dhidi ya wageni wao hao baada ya mchezo uliopita kwenye Uwanja wa Kumbukumbu ya Karume kushinda kwa mabao 2-0, Biashara iliyoshuka dimbani mara 23 kama ilivyo kwa 'Wekundu' hao, yenyewe ipo nafasi ya tisa ikiwa na alama 32.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >